**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI**

# SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI - ZANZIBAR

**2022**

## DIBAJI


Zanzibar ina historia ya muda mrefu ya kuhamasisha na kuimarisha shughuli mbali mbali za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwemo kuweka mikakati ya Kitaifa na Kisekta inayosimamia masuala ya uwezeshaji nchini ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu na miongozo ya kutekeleza programu hizo. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufanya jitihada mbali mbali za kuimarisha maisha na ustawi wa raia wake kwa kuimarisha uchumi na kuweka programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umekuwa ni kitovu cha mabadiliko na suluhisho la kupambana na tatizo la umasikini na ukosefu wa ajira hasa kwa Vijana.

Utafiti wa Nguvu Kazi wa mwaka 2021 umebainisha kwamba Zanzibar ina asilimia 19.7 ya ukosefu wa ajira nchini ambapo kwa Vijana (miaka 15-35) ni asilimia 27.6. Ili kupambana na changamoto hii, Serikali kupitia Dira 2050 na Mkakati wake wa utekelezaji umeainisha vipaumbele vya Serikali katika kukuza Uchumi na kuinua kipato cha Mwananchi ikiwemo kuikuza Sekta ya Uchumi wa Buluu, Utalii, kuimarisha Uwekezaji na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi nchini kupitia sekta hizo kuu.

Mbali na jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo ukosefu wa fedha au mitaji ya kutosha kuimarisha bidhaa za wajasiriamali, mazingira bora ya biashara, miundombinu hafifu ya uwezeshaji, kutokuwepo na miongozo ya uratibu, masoko ya bidhaa za wajasiriamali, mafunzo na ushindani wa kibiashara pamoja na mifumo thabiti ya kitaasisi na kisheria inayosimamia masuala ya uwezeshaji nchini.

Changamoto hizo zinahitaji kuwekewa Mifumo ya Kisera na Kisheria ili ziweze kutatuliwa. Hivyo, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar inalenga kuratibu na kuweka mazingira mazuri kwa watu wote wa Zanzibar wakiwemo Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu kushiriki katika shughuli za uwezeshaji, kusimamia na kuzitumia fursa za uchumi zilizopo kwa maslahi yao na maendeleo ya nchi yao.

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inawaomba Watendaji wote, Wananchi, Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo kusimamia utekelezaji wa malengo na mikakati iliyoainishwa katika Sera hii ili kuinua hali za Wananchi Kiuchumi na hatimae kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi.



……………………………………………

**MHE. MUDRIK RAMADHAN SORAGA**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI ZANZIBAR.**

## SHUKRANI

Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji imeandaa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kuweka Muongozo utakaosaidia kuweka uratibu mzuri wa kusimamia utekelezaji wa Shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwemo kuimarisha Mifumo ya Kitaasisi na Kisheria. Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi imeandaliwa kwa Mashirikiano na Taasisi mbali mbali zinazosimamia masuala ya Uwezeshaji nchini ili kubaini na kuzitatua changamoto zinazoikabili sekta hii kwa pamoja. Hivyo, ARKUU inapenda kuwashukuru wote kwa jitihada na michango yao ambayo imefanikisha kuanzishwa kwa Sera hii ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.

Shukrani za kipekee ziende kwa timu ya Wataalamu kutoka Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ikiongozwa na Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti akishirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa kuandaa na kuhakikisha kwamba mafanikio yanapatikana kuanzia hatua ya utayarishaji hadi kumalizika kwa Sera hii na kuifanya iendane na ikubalike kimuundo na kimtiririko kama inavyoonekana sasa. Pia, tunazishukuru Taasisi za Wajasiriamali zilizoshirikiana nasi katika kuandaa Sera hii.

Aidha, Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inatambua na kuthamini michango ya Wadau wote zikiwemo Taasisi za Kijamii, Washirika wa Maendeleo na Watu Binafsi ambao kwa namna moja au nyingine wamefanikisha kuwepo kwa Sera hii ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ni vigumu kuwataja mmoja mmoja katika mchakato huu mrefu wa kuandaa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi lakini kwa niaba ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kabisa kwa Wadau wote na tunaithamini sana michango yao mikubwa katika kukamilisha mchakato mzima wa uundwaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ni matuamini kila Mdau atasimamia utekelezaji wa eneo lake la Sera ili tuweze kufikia Malengo na Dira tuliyoitarajia kwa pamoja.



………………………………

**DKT. ISLAM SEIF SALUM**
**KATIBU MKUU (KAZI NA UWEZESHAJI),**
**AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI,**
**ZANZIBAR.**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AMPR-SUB | Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi |
| ARKUU | Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji |
| AZAKI | Asasi za Kiraia |
| BDSs | Business Development Support Services (Huduma za Maendeleo ya Biashara) |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| COSTECH | Commission for Science and Technology (Tume ya Sayansi na Teknolojia) |
| EBDs | Entreprenuership Business Development Services (Vituo vya Huduma za Biashara na Ujasiriamali) |
| GDP | Gross Domestic Product (Pato la Ndani) |
| HBS | House Hold Budget Survey (Utafiti wa Matumizi ya Kaya) |
| ILFS | Integrated Labor Force Survey (Utafiti wa Nguvukazi) |
| MKUZA | Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar |
| MSMEs | Micro, Small and Medium Enterprises (Wajasiriamali Wadogo wadogo, Wadogo na wa Kati) |
| OCGS | Office of Chief Government's Statistian (Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali) |
| PWDs | People with Disabilities (Watu Wenye Ulemavu). |
| SACCOS | Saving and Credit Cooperative Societies (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Kukopa) |
| SADC | Southern Africa Development Cooperation (Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika) |
| SDGs | Sustainable Developments Goals (Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia) |
| SIDP | Sustainable Industrial Development Programmes |
| SMEs | Small and Medium Enterprises (Wafanyabiashara Wadogo na wa Kati) |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| VVU | Virusi Vinavyosababisha UKIMWI |

| | |
|---|---|
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |
| ZBS | Zanzibar Bureau of Standards (Taasisi ya Viwango Zanzibar) |
| ZFDA | Zanzibar Food and Drugs Agency (Wakala wa Dawa, Chakula na Vipodozi Zanzibar) |
| ZTBI | Zanzibar Technology Business Incubation (Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali) |
| ZYEAP | Zanzibar Youth Employment Action Plan (Mpango Kazi wa Ajira kwa Vijana Zanzibar) |

## MAANA YA MANENO

| | |
|---|---|
| **Masoko** | Ni maeneo ambayo wanunuzi na wafanyabiashara wanakutana ili kuuza na kununua bidhaa/huduma. Aidha, inahusisha taaluma pamoja na taratibu zinazohusiana na jinsi ya kutayarisha na kuuza bidhaa zinazozalishwa. |
| **Mitaji** | Ni rasilimali zinazotumika katika kuanzisha au kuendeleza miradi ya Kiuchumi ikiwemo fedha na vifaa. |
| **Mjumuiko wa Taasisi za Kifedha** | Ni upokeaji wa huduma za Kifedha katika gharama nafuu kwa sehemu za wasiojiweza na makundi ya jamii yenye vipato vya chini. |
| **Muundo wa kusaidia kukuza biashara** | Ni mfumo/chombo ambacho kinasaidia uwezeshaji kiuchumi kama vile vituo vya kulea na kukuza wajasiriamali/biashara na huduma za kitaalamu za maendeleo ya biashara. |
| **Shughuli za Uwezeshaji Kiuchumi** | Ni kujenga fursa kwa matumizi ya rasilimali za ndani katika namna yenye tija na ufanisi. |
| **Udhibiti Ubora** | Ni tendo la kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma za kampuni fulani zinaandaliwa na kutolewa kwa Wateja/walaji kwa viwango stahiki, kwa muda muafaka na kwa gharama inayokidhi (nafuu). |
| **Ujasiriamali** | Ni namna ya kubuni na kufanikisha uletaji na utoaji wa huduma au bidhaa Fulani yenye manufaa kwa walengwa na walengwa hao wakalipia hiyo huduma/bidhaa. |
| **Utamaduni wa kiujasiriamali** | Ni ile hali ambayo mtu anahamasishwa kuvumbua, kutengeneza na kujaribu bila uoga kufanya jambo. |
| **Uwezeshaji Kiuchumi** | Ni hali au matendo ya kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kushiriki katika shughuli za kiuchumi kwa tija |
| **Wafanyabiashara** | Ni watu wanaojihusisha na biashara ndogo ndogo na kiwango cha kati. Inahusisha wafanyabiashara wadogo, wadogo wadogo na wa kati |
| **Watu Wenye Mahitaji Maalumu** | Ni watu walio katika kundi la Wanawake, Vijana, Wazee, Watu Wenye Ulemavu, Watu wanaoishi na VVU/UKIMWI na wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. |

## YALIYOMO

DIBAJI ........ i

SHUKRANI ........ ii

ORODHA YA VIFUPISHO ........ iii

MAANA YA MANENO ........ v

YALIYOMO ........ vi

SURA YA KWANZA ........ 1

1.0 UTANGULIZI ........ 1

1.1. Usuli ........ 1

1.2. Haja ya Kuwa na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. ........ 2

1.3. Upeo wa Sera ........ 4

1.4. Uhusiano Uliopo Kati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sera Nyengine za Kisekta, kimataifa na kikanda. ........ 5

1.4.1. Sera ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar (2002) ........ 6

1.4.2. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar (2005) ........ 6

1.4.3. Sera ya Uwekezaji ya Zanzibar (2005) ........ 6

1.4.4. Sera ya Maendeleo ya Vijana (2005) ........ 6

1.4.5. Sera ya Zanzibar ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs 2006) ........ 7

1.4.6. Sera ya Biashara ya Zanzibar (2006) ........ 7

1.4.7. Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006) ........ 7

1.4.8. Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar (2008) ........ 8

1.4.9. Sera ya Ajira ya Zanzibar (2009) ........ 8

1.4.10. Sera ya Maendeleo ya Mifugo Zanzibar (2011) ........ 8

1.4.11. Sera ya Afya ya Zanzibar (2011) ........ 9

1.4.12. Sera ya Ushirika ya Zanzibar (2014) ........ 9

1.4.13. Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar (2014) ........ 9

1.4.14. Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar (2014) ........ 10

1.4.15. Sera ya Jinsia Zanzibar (2016) ........ 10
1.4.16. Sera ya Afya na Usalama Kazini (2017) ........ 10
1.4.17. Sera ya Taifa ya Ardhi Zanzibar (2018) ........ 10
1.4.18. Sera ya Utalii Zanzibar (2018) ........ 11
1.4.19. Sera ya Michezo ya Zanzibar (2018). ........ 11
1.4.20. Sera ya Diaspora Zanzibar (2018) ........ 12
1.4.21. Sera ya Watu Wenye Ulemavu (2018) ........ 12
1.4.22. Sera ya Viwanda ya Zanzibar (2019) ........ 12
1.4.23. Sera ya Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo Wadogo (2019) ........ 12
1.4.24. Sera ya Uchumi wa Buluu (2022) ........ 13
SURA YA PILI ........ 14
**2.0** HALI HALISI ........ 14
2.1 Muktadha wa Kijamii na Kiuchumi ........ 14
2.1.1. Miundo mbinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. ........ 15
2.2. Mafunzo ya Uwezeshaji. ........ 17
2.2.1. Fikra Mgando ........ 18
2.2.2. Utamaduni wa Ujasiriamali na Uwezo ........ 19
2.2.3. Muundo wa kusaidia Kukuza Biashara ........ 19
2.3. Upatikanaji wa Masoko ........ 20
2.3.1. Udhibiti Ubora ........ 21
2.3.2. Mnyororo wa Thamani ........ 22
2.3.3. Makongano ya Kiuchumi ........ 23
2.3.4. Ununuzi ........ 23
2.4 Fedha na Mitaji ya Uwezeshaji. ........ 23
2.5 Ajira na Fursa za Ajira ........ 25
2.5.1 Elimu ........ 26

2.5.2 Uchumi wa Buluu ........ 26
2.5.3 Uwekezaji ........ 27
2.5.4 Utalii ........ 28
2.5.5 Kilimo ........ 28
2.5.6 Viwanda. ........ 29
2.6 Ubunifu na Kuasili Teknolojia ya Kisasa ........ 30
2.7 Muundo wa Kitaasisi na Uratibu ........ 30
2.8 Mifumo ya Kisera na Kisheria ........ 31
2.9 Masuala Mtambuka ........ 31
2.9.1 Jinsia ........ 31
2.9.2 Vijana ........ 32
2.9.3 VVU/UKIMWI na Dawa za Kulevya ........ 32
2.9.4 Watu Wenye Ulemavu ........ 33
2.9.5 Mabadiliko ya Tabia nchi na Mazingira. ........ 33
2.9.6 Ongezeko la Idadi ya Watu ........ 33
2.9.7 Wazee ........ 34
SURA YA TATU ........ 35
3.0 DIRA, DHAMIRA NA KANUNI ELEKEZI ZA SERA ........ 35
3.1 Dira ........ 35
3.2 Dhamira ........ 35
3.3 Lengo Kuu ........ 35
3.4 Malengo Mahususi ........ 35
3.5 Kanuni Elekezi za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ........ 36
SURA YA NNE ........ 38
4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA ........ 38
SURA YA TANO ........ 43

5.0 UTARATIBU WA KITAASISI KATIKA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR ........................ 43

5.1 Mfumo wa Kitaasisi Katika Utekelezaji wa Sera .................................................... 43

5.2 Muundo wa Kitaasisi ............................................................................................... 43

5.3 Mfumo wa Kisheria .................................................................................................. 44

5.4 Mfumo wa Uratibu.................................................................................................... 44

5.5 Majukumu ya Wadau katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ........................................................................................ 45

5.5.1 Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. .................................. 45

5.5.2 Majukumu ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi............................... 46

5.5.3 Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala........................................................................... 46

5.5.4 Wizara inayohusika na Fedha ................................................................................ 47

5.5.5 Tume ya Mipango. .................................................................................................. 47

5.5.6 Wizara inayohusika na Uchumi wa Buluu na Uvuvi ........................................... 48

5.5.7 Wizara inayohusika na Ufugaji na Kilimo........................................................... 48

5.5.8 Wizara inayohusika na Biashara na Viwanda...................................................... 49

5.5.9 Wizara inayohusika na Elimu ................................................................................ 49

5.5.10 Wizara inayohusika na Vijana na Wanawake...................................................... 50

5.5.11 Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ .................... 50

5.5.12 Wizara inayohusika na Utalii.................................................................................. 50

5.5.13 Wizara inayosimamia Watu wenye Ulemavu. ...................................................... 51

5.5.14 Wizara inayohusika na Afya ................................................................................... 51

5.5.15 Sekta Binafsi ............................................................................................................ 51

5.5.16 Asasi za Kiraia ......................................................................................................... 52

5.5.17 Vyombo vya Habari ................................................................................................ 52

5.5.18 Taasisi za Kifedha.................................................................................................... 52

5.5.19 Washirika wa Maendeleo......................................................................................... 53

SURA YA SITA ........................................................................................................ 54
6.0 Ufuatiliaji na Tathmini ........................................................................................ 54
6.1 Ufuatiliaji ........................................................................................................ 54
6.2 Tathmini ........................................................................................................ 54
6.3 Utaratibu wa Kuripoti ........................................................................................ 55
6.4 Mkakati wa Mawasiliano ........................................................................................ 55
6.5 Mpango wa Rasilimali wa Sera ........................................................................................ 55

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Usuli

Kihistoria uchumi wa Zanzibar ulikuwa unamilikiwa na watawala wa kikoloni kabla ya Mapinduzi ya mwaka 1964. Wananchi hawakupata fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kulazimika kujishughulisha na vibarua na kazi za sekta isiyo rasmi. Hata hivyo walioingia katika sekta hiyo walifanya biashara duni sana na hawakupata fursa yoyote ya kuwezeshwa ili kukuza biashara na shughuli walizokuwa wakizifanya. Fursa za kiuchumi kwa zama hizo zilitolewa zaidi kwa makundi ya watawala.

Mara baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilichukua hatua mbali mbali ambazo zilikuwa na lengo la kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kiuchumi na kijamii ili kuimarisha ustawi wao. Miongoni mwa hatua hizo ni pamoja na kuunda Wizara ya kuweka hali za Wananchi sawa, kutoa huduma zote za msingi bila ya malipo, kugawa ardhi eka tatu tatu kwa ajili ya kilimo na kadhalika. Pamoja na huduma na fursa hizo zilizotolewa kwa wananchi, ushiriki wao katika uchumi na uzalishaji ulibaki kuwa mdogo na hali ya umasikini miongoni mwa jamii iliongezeka. Mipango mbali mbali iliandaliwa ya kupambana na umasikini, kutokana na mipango hiyo, dhana ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ilibuniwa ili wananchi wa kawaida waweze kuzalisha na kujikimu na familia zao kwa kuanzisha biashara na hatimae kuchangia katika Pato la Taifa.

Mnamo mwaka 1967, Idadi ya watu Zanzibar ilikuwa ni 354,815 (Sensa 1967). Mwaka 1978, ongezeko la watu lilikuwa kwa kiwango cha asilimia 2.7 ambacho kiliongezeka hadi kufikia asilimia 3.1 mwaka 2002 na baadae kushuka hadi kufikia asilimia 2.8 mwaka 2012. Kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya mwaka 2012, idadi ya watu iliongezeka na kufikia watu 1,303,569, ikiwa ni wastani wa ongezeko la asilimia 2.8 kwa mwaka. Miaka mitano baadae (mwaka 2017), idadi ya watu ilikadiriwa kuwa 1,534,271 ambapo kati ya idadi hiyo, 788,422 ni Wanawake ambao ni sawa na asilimia 51.4 na 745,849 ni Wanaume ambao ni sawa na asilimia 48.6.

Mwaka 2020, makadirio ya idadi ya watu yameonesha kuwa Zanzibar ina jumla ya watu 1,671,598 kati yao 857,439 sawa na asilimia 51.3 ni Wanawake na watu 814,159 ni wanaume sawa na asilimia 48.7(OCGS 2020). Idadi hii inaonesha ongezeko la watu wanaokaa katika kila kilomita moja ya mraba kufikia watu 603 mwaka 2020, kutoka watu 530 mwaka 2012. Mwaka 2021 idadi ya watu wa Zanzibar inakadiriwa kufikia watu 1,717,608 ambapo watu 837,034 sawa na asilimia 48.7 ni wanaume na watu 880,574 sawa na asilimia 51.3 ni Wanawake

Kwa Mujibu wa Makadirio ya idadi ya watu kwa mwaka 2020, idadi ya Vijana wenye umri miaka 15 hadi 35 kwa Zanzibar ni 590,885 sawa na asilimia 35.4 ambapo wanaume ni 281,773 sawa na asilimia 47.7 na Wanawake ni 309,112 sawa na asilimia 52.3. Nguvu kazi ya Taifa, watu wenye umri kati ya miaka 15 hadi 64 ni asilimia 76 ya watu wote. Mbali na

nguvu kazi hiyo kuna asilimia 2.7 ya Wazee wemye umri wa zaidi ya miaka sitini ambao nao kwa malengo ya sera hii wanahitaji huduma za uwezeshaji kiuchumi pamoja na hifadhi ya jamii.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mikakati mbali mbali ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi miongoni mwa watu wa Zanzibar, mikakati ambayo pamoja na malengo mengine inalenga kukuza ajira nchini. Mikakati hii imeelezwa vyema katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo 2026, Dira ya Zanzibar 2050 na Mpango Kazi wa Ajira kwa Vijana wa Zanzibar (ZYEAP 2014-18) ambayo inasisitiza mahitaji ya kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira kupitia juhudi za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Pia, imeweka Wizara Maalum ambayo inahusika na kuwezesha wananchi kiuchumi.

Katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) msisitizo umewekwa katika kuwawezesha watu kwa ajili ya Maendeleo. Lengo la Kwanza, lengo la Nne na lengo la Tano yanahusiana moja kwa moja na masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi; lengo la Tano ni mahususi kwa kuwawezesha Wanawake na Wasichana Kiuchumi na kupambana na ukatili dhidi ya Wanawake na Wasichana. Agenda 2063, 'Afrika tuitakayo' katika eneo lake la kwanza linasisitiza masuala ya kukuza uchumi na kuwawezesha wananchi kiuchumi pamoja na kuziimarisha sekta kuu za kiuchumi ikiwemo Uchumi wa Buluu.

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni mchakato unaohusisha matendo ya makusudi ya Serikali kwa kushirikiana na Wadau wengine ya kuongeza ajira na vipato kwa watu wake kwa kuimarisha nafasi na hadhi za kiuchumi za Wanawake, Wanaume, Vijana na makundi mengine maalumu yenye changamoto za kipato. Pia, inahusisha kuimarisha namna ya kuzifikia fursa za upatikanaji wa ajira, kuzifikia huduma za kifedha, ujuzi wa maendeleo, mgawanyo wa manufaa ya ukuaji, upatikanaji na udhibiti wa uzalishaji wa rasilimali, upatikanaji wa soko/taarifa za masoko, uvumbuzi, ubunifu na teknolojia.

Kwa hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wadau wengine wanahakikisha kwamba Mikakati madhubuti inaandaliwa, kuendelezwa na kutekelezwa ili kukidhi malengo ya kuyawezesha makundi yote ya jamii ya Zanzibar na kuongeza ajira na vipato vya wananchi, kujenga uwezo na kuongeza ujuzi wa kutumia fursa za kiuchumi zilizopo.

### 1.2. Haja ya Kuwa na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar.

Zanzibar ni miongoni mwa nchi zinazoendelea ambayo inakabiliwa na changamoto mbali mbali za kiuchumi kutokana na uhaba wa rasilimali za kiuchumi, uwezo mdogo wa fursa za kiuchumi, pamoja na wingi wa watu masikini wasio na uwezo wa kupata mahitaji yao ya lazima. Kwa Mujibu wa Takwimu za Utafiti wa Matumizi ya Kaya (*Household Budget Survey -HBS, 2019/20),* asilimia 25.7 ya idadi ya watu Zanzibar inaishi chini ya mstari wa umasikini**,** yaani wasioweza kupata mahitaji muhimu na kiwango cha Umasikini wa Chakula ni asilimia 9.3 hii ni kwa sababu ya mfumuko wa bei ya juu ya vyakula (ambayo ni kwa wastani wa asilimia 7.4 kwa mwaka) ilifanya watumiaji wenye kipato kidogo ambao mapato yao hayakuendana na kupanda kwa bei washindwe kumudu bidhaa hiyo. Hali hii ya

umasikini ilikuwa mbaya zaidi mnamo mwaka 2014/2015 ambapo asilimia ya watu masikini wa kushindwa kumudu mahitaji ya lazima ilikuwa asilimia 30.4 na idadi ya watu masikini wa chakula ilikuwa ni asilimia 10.8.

Kiwango cha ukosefu wa Ajira miongoni mwa Vijana wa kati ya umri wa miaka 15–34 kimeongezeka na kufikia asilimia 27.4 kwa mujibu wa taarifa za awali za Utafiti wa nguvu kazi ya Taifa (ILFS 2021). Tatizo hili la ukosefu wa ajira linahitaji muongozo wa Sera itakayoweka wazi na kubainisha mikakati ya kujihusisha kikamilifu katika sekta isiyo rasmi na kutengeneza ajira zaidi ili kufikia lengo la kuzalisha ajira laki tatu katika kipindi hiki cha utekelezaji wa sera hii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Kufuatia hali hiyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuandaa Mipango mahasusi ya kupambana na umasikini. Mipango hiyo inalenga kusaidia wananchi kuondokana na umasikini wa kipato na mahitaji ya lazima pamoja na ule wa chakula. Kupitia katika mipango hiyo kulianzishwa programu za kuwezesha wananchi kiuchumi ili kuondoa Umasikini Zanzibar. Hivyo**,** Sera hii inatekeleza kwa vitendo maazimio yaliyopo katika Dira 2050. Pia, Sera hii inatafsiri kwa vitendo utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) na Ajenda 2063 ‘Afrika tuitakayo’ ambazo kwa pamoja zinasisitiza juu ya kuiwezesha jamii kiuchumi ili kusiwe na ~~n~~Nchi itakayoachwa nyuma kimaendeleo. Aidha, Malengo endelevu ya Dunia inakusudia kila Nchi ifurahie ukuaji endelevu wa kiuchumi na maendeleo na kila nchi izalishe ajira zenye staha kwa wote.

Ukuaji wa Uchumi wa Zanzibar bado uko chini, haujaweza kupunguza umasikini wa wananchi kwa kiwango kinachotarajiwa, malengo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ni kuwajengea uwezo ili waweze kujikimu, waongeze uzalishaji na kuhakikisha Uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa upo mikononi mwa wananchi wenyewe. Idadi kubwa ya wananchi bado ni masikini kwa hivyo maelekezo ya sera hii ni kuwainua wananchi wanyonge kutoka kufikiria kujikimu kwa chakula na kuweza kuzalisha kibiashara na kuwekeza kwenye shughuli zenye tija zaidi. Pia, kuyawezesha makundi ya wananchi wenye kipato cha kati na cha juu kuanzisha viwanda na biashara nyengine ili waweze kutoa ajira kwa wananchi wenzao.

Mabadiliko makubwa ya kiuchumi na teknolojia yametoa fursa na nafasi kwa watu wengi zaidi kuingia kwenye ujasiriamali na kufanikiwa. Mbali na ukosefu wa ajira, maendeleo ya kiteknolojia yamerahisisha sana ujasiriamali. Pamoja na fursa hizi zinazowavutia wananchi kuingia kwenye biashara na ujasiriamali bado sio wote wanaopata mafanikio makubwa. Wananchi wengi wanaoingia kwenye ujasiriamali au wanaoanza biashara, biashara zao zinaishia kufa ndani ya muda mfupi na wale ambao biashara zao hazifi, zinaishia kudumaa na kushindwa kukua zaidi. Sera hii itatoa ufumbuzi wa changamoto zote hizo. Vile vile, Mfumo wa elimu uliopo haumpi kijana fursa ya kuweza kujiajiri pindi anapomaliza elimu yake ya msingi na soko rasmi la ajira haliwezi kuchukua Vijana wote wanaomaliza elimu yao ya msingi, hivyo Sera hii itatoa Muongozo wa namna ya kukabiliana na kundi hili la Vijana nchini**.** Mbali na hayo, Vijana wengi wanazalisha huduma na bidhaa mbali mbali lakini

wanakosa soko lenye tija na la kudumu.  Hali hii inachangiwa na ukosefu wa muongozo katika kushughulikia suala hili.

Programu na Taasisi tofauti zimeanzishwa ikiwa ni jitihada za Serikali za kuwawezeha wananchi kiuchumi. Programu hizo zinajumuisha utoaji wa mafunzo, mikopo, ruzuku, vifaa vya kazi na huduma za masoko. Hata hivyo, jitihada hizi zilikosa uratibu sahihi na hivyo hazikuweza kufikia malengo yaliyotarajiwa. Shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinatekelezwa kupitia Taasisi na mifumo tofauti jambo ambalo imepelekea shughuli hizo kukosa uratibu mzuri na wakati mwengine shughuli za aina moja zinafanywa na Taasisi tofauti kwa walengwa hao hao, hali hii ilipelekea kupoteza rasilimali chache zilizopo bila kufikia malengo. Hivyo, kutokana na changamoto hizi, Serikali imeona haja ya kufanya mapitio ya Sera ya Uwezeshaji Kiuchumi ya mwaka 2019 na kuwa Sera ya Taifa itakayosimamia masuala yote ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi chini ya Taasisi moja.

Sera hii itakuwa ndiyo muongozo elekezi na itakayosimamia na kuratibu shughuli za Taasisi ya Kitaifa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. Aidha, itaondosha changamoto za uratibu na utekelezaji wa shughuli na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilizopo na kuleta mabadiliko kwa Vijana, Wanawake na Makundi mengine yenye mahitaji ya uwezeshaji kwa wananchi wa Zanzibar yakiwemo makundi yenye mahitaji maalumu. Itaunganisha shughuli zinazofanana za uwezeshaji katika sekta nyengine ili kuleta maendeleo endelevu katika sura na muenekano wa Kitaifa.

### 1.3. Upeo wa Sera

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni miongoni mwa sera zilizotayarishwa na Serikali kwa ajili ya kuweka mazingira mazuri kwa wananchi kuweza kufanya shughuli zao za kiuchumi kwa ufanisi.  Sera hii itatekelezwa katika maeneo yote ya Unguja na Pemba ingawa pia inatoa fursa ya mashirikiano ya utekelezaji wa mikakati ya sera na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na washirika wa Maendeleo.

Katika mfumo wa Serikali, Sera hii inajumuisha na kushirikisha Taasisi mbali mbali za Serikali kupitia sera, mipango na programu mbali mbali za kwawezesha wananchi kiuchumi kwa lengo la kuunganisha nguvu ya pamoja ili kutimiza malengo ya sera. Aidha, Taasisi zisizokuwa za Serikali nazo zitafanya kazi za kuwawezesha wananchi kiuchumi kwa kuzingatia maelekezo ya ushauri wa kisera.

Wananchi wa rika mbali mbali watahudumiwa kulingana ma malengo ya sera, zaidi ni watu wenye umri wa kufanyakazi, lakini pia Wazee wenye umri mkubwa watapatiwa huduma za uwezeshaji kwa kuzingatia maelekezo ya sera hii kwa kipindi cha miaka kumi ijayo.

## 1.4. Uhusiano uliopo kati ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Sera Nyengine za Kisekta, K~~k~~imataifa na K~~k~~ikanda.

Dira ya Zanzibar ya Mwaka 2050 na Mkakati wake wa utekelezaji inaeleza wazi umuhimu wa kuwawezesha wananchi wa Zanzibar Kiuchumi. Miongozo hii pamoja na hatua zake za mwanzo hadi matokeo yake ya msingi imepambanua mahitaji na mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuweza kufikia lengo la kuongeza ukuaji wa kiuchumi na kuondoa umasikini miongoni mwa wananchi wake. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inaazimia kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025 katika Ibara ya 139 inayohusu Mageuzi ya Kiuchumi, Ibara ya 142 ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kupambana na Umasikini, Ibara ya 144 ya Sekta ya uzalishaji mali, Ibara ya 148 Uvuvi na Mazao ya Baharini, Ibara ya 152 Utalii, Ibara ya 156 Viwanda na Biashara, Ibara ya 158 Huduma za Fedha, Ibara ya 160 Vyama vya Ushirika na Ibara ya 162 inahusu Uchumi wa Buluu.

Dira 2050 na Mpango wake wa utekelezaji unatafsiri kwa vitendo na unakwenda sambamba na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ambayo yanasisitiza haja ya kuwepo kwa ukuaji wa Kiuchumi kwa kuondoa umasikini wa aina zote, pia inatambua maendeleo na mchango wa MSMEs katika kuleta mafanikio ya malengo yaliyowekwa na Mkakati huu. Mpango huo umeainisha Miradi mbali mbali ya usarifu wa mazao ya sekta ya kilimo, uvuvi, mifugo, huduma za sekta ya utalii na usarifu wa bidhaa mbali mbali ambazo ni sekta za kipaumbele kwa ajili ya sekta binafsi/MSMEs na nchi ikiwemo Uchumi wa Buluu. Ili sekta hizo za kipaumbele ziweze kutekeleza shughuli zake kwa ufanisi, kuna umuhimu kwa wananchi kuwezeshwa ili waweze kufanya kazi zao kwa tija. Uwezeshaji kupitia Taasisi ndogo ndogo za ushirika na vikundi vya uzalishaji ni muhimu ili kuwashirikisha wananchi wengi katika utaratibu wa uwezeshaji kwa wakati mmoja.

Agenda 2063 katika eneo lake la kwanza la kipaumbele limetilia mkazo katika kuimarisha sekta za kiuchumi kwa nchi wanachama ambapo linatilia mkazo umuhimu wa kuimarisha sekta za Uchumi wa Buluu, Kilimo, Elimu, Ustawi wa Jamii na eneo la sita linalotilia mkazo usawa wa kijinsia na kuwawezesha Vijana na Wanawake.

Mkataba wa Kimataifa wa Kupinga aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (1979) pamoja na mambo mengine unatilia mkazo kwa kiasi kikubwa katika kuwawezesha Wanawake katika nyanja zote za kiuchumi na kijamii pamoja na kupinga aina zote za udhalilishaji miongoni mwa nchi wanachama. Kwa kuwa suala la uwezeshaji ni mtambuka, utekelezaji wake unahitaji muunganiko na mahusiano kati ya sekta mbali mbali. Kwa maana hiyo sera hii ya uwezeshaji ina mahusiano makubwa na Mikataba ya Kimataifa na Maazimio ya Kikanda yanayosimamia shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mbali na Mikataba ya Kimataifa, Maazimio ya Kikanda na Mipango ya Kimataifa, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina mahusiano ya karibu katika utekelezaji wake na Sera mbali mbali za Kisekta kama ifuatavyo:-

### 1.4.1. Sera ya Maendeleo ya Kilimo Zanzibar (2002)

Sera ya Maendeleo ya Kilimo ya Zanzibar (2002) inasisitiza uwekwaji wa mazingira mazuri ili kuhamasisha Uwekezaji katika shughuli za kilimo. Hii ni katika kutambua maeneo muhimu ya kuwekeza katika kilimo na umuhimu wa kuongeza thamani ya mazao na malighafi zilizopo ukianzia na aina mbalimbali za viungo na matunda yanayo patikana ndani ya Nchi na mahitaji ya kuendeleza huduma ya usambazi wa chakula kwa ukuaji wa Sekta ya Utalii. Wananchi wengi wa Zanzibar hasa wa vijijini wamewekeza nguvu zao katika kilimo, lakini kwa asilimia kubwa wanalima kilimo duni cha kujikimu ambacho hupata mavuno haba ya chakula cha siku chache tu. Hata hivyo sekta hii ya kilimo inabaki kuwa muhimu kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa ajili hiyo uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia sekta ya kilimo ni jambo la lazima ili kuongeza uzalishaji katika sekta hiyo, kutoka kilimo cha kujikimu kwenda katika uzalishaji wa kibiashara. Mashirikiano ya sera hizi yatasaidia ongezeko la pato la Taifa na ukuaji wa uchumi.

### 1.4.2. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar (2005)

Mafunzo ya Ufundi ni njia muhimu kuelekea kupunguza umasikini kwa kuwa inatoa fursa za kujiajiri. Lengo kuu la Sera ni kutoa wigo wa fursa za kujifunza kwa Vijana ili kutengeneza fursa za ajira na kukuza thamani ya ujasiriamali na ujuzi. Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar inatoa fursa kwa Vijana waliopata ujuzi katika vituo vya mafunzo ya amali kuweka mifumo sahihi na kuwapatia nyenzo tayari kuingia katika uzalishaji katika fani mahsusi kulingana na ujuzi wao.

### 1.4.3. Sera ya Uwekezaji ya Zanzibar (2005)

Sera ya Uwekezaji ya Zanzibar imeainisha malengo ya jumla ya Sera ambayo yameelekezwa katika sekta za vipaumbele ambazo ni pamoja na huduma za biashara na fedha, Bandari huru na kukuza Sekta ya Utalii kama msingi wa Maendeleo mijini na vijijini; utengenezaji hasa wa bidhaa za kusafirishwa na kuuzwa Nje ya nchi (na msisitizo upo kwenye SMEs); na kuendeleza Sekta ndogo ndogo za uvuvi na bahari na biashara ya bidhaa na huduma. Sekta zote hizi za kipaumbele kwenye sera ya uwekezaji zinaweza kuendelezwa na wananchi waliowezeshwa katika maeneo hayo. Sera ya uwezeshaji itachukuwa nafasi yake kuwawezesha wananchi kushiriki katika uwekezaji ili kuwapa fursa wananchi kutumia rasilimali zao kuwekeza na kutumia fursa za uwekezaji mkubwa katika maeneo yao kwa ajili ya kukuza uchumi wao na kuchangia katika uchumi wa nchi.

### 1.4.4. Sera ya Maendeleo ya Vijana (2005)

Sera ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka (2005) imeandaliwa na Serikali kwa ajili ya kusimamia maslahi ya Vijana. Sera hii inalenga kusimamia masuala ya maendeleo ya Vijana ambayo ni pamoja na elimu, mafunzo ya amali, ujasiriamali, ajira, ushiriki na ushrikishwaji. Sera ya Maendeleo ya Vijana inatoa muongozo utakaoimarisha ustawi wa Vijana kati ya miaka 15 hadi 35 katika kukabiliana na changamoto mbali mbali za kiuchumi na kijamii ikiwemo ukosefu wa ajira, athari za dawa za kulevya, UKIMWI na umuhimu wa ushiriki na ushirikishwaji wao katika mipango mbali mbali ya maendeleo. Sera ya Maendeleo ya Vijana

imeweka utaratibu wa kuanzisha Baraza la Vijana katika ngazi ya shehia hadi Taifa. Baraza la Vijana Zanzibar ni Jukwaa rasmi linalowaunganisha Vijana wote bila ya kuangalia mtazamo wa kisiasa au dini katika kuelelezea na kutetea maslahi yao kiuchumi na kijamii. Sera hii imebainisha mikakati tofauti ya kuwawezesha Vijana kiuchumi kupitia sekta na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo nchini.

### 1.4.5. Sera ya Zanzibar ya Wajasiriamali Wadogo na wa Kati (SMEs 2006)

Sera hii imeandaliwa kusaidia kuunganisha Sera na mikakati iliopo yenye lengo la kukuza sekta ya wajasiriamali wadogo na wa kati, kuendeleza biashara ndogo ndogo na ujuzi wa kiufundi miongoni mwa Watendaji, watunga sera na wanufaika wa sera hii hapa Zanzibar, ili kusaidia wajasiriamali kupitia ajira na huduma zao, kuongeza thamani za mazao kwa makongano yaliyokusudiwa, kuimarisha sekta za kifedha, kukuza msingi wa kodi na kuwezesha uwekezaji wa kifedha, uzalishaji na ukuaji wa viwanda vidogo vidogo. Maendeleo ya Sekta na uanzishaji/uimarishaji wa makongano ya biashara unachukuliwa kama moja kati ya njia bora ya kutia moyo na kusaidia ushirikiano kati ya Taasisi na Taasisi, wajasiriamali wenyewe kwa Maendeleo ya nchi.

Sera hii ina mahusiano na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwani walengwa wake wakuu ni wafanyabiashara ndogo ndogo na za kati (SMEs). Mgawanyo wa biashara hizi katika sera ya SMEs utasaidia sana utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuwawezesha wananchi kwa mujibu wa mahitaji ya makundi ya walengwa husika.

### 1.4.6. Sera ya Biashara ya Zanzibar (2006)

Sera ya Biashara ya Zanzibar imetayarishwa na kupendekeza utekelezwaji wa taratibu za kuzijengea uwezo biashara, ikiwa na msisitizo kwenye kuondoa vikwazo vya usambazaji na upatikanaji wa bidhaa mbali mbali kwa ubora wa bidhaa kuzingatia wananchi. Pia, Sera ina lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara nchini pamoja na kuzingatia masuala kufanya biashara na mataifa ya nje. Mahusiano ya Sera ya Biashara Zanzibar na Sera ya Taifa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yapo katika malengo ya kusaidia wafanyabiashara kufanya kazi zao vizuri ili kuchangia maendeleo ya nchi. Mikakati ya Sera ya Biashara juu ya udhibiti wa viwango na upatikanaji wa masoko ni muhimu sana kuzingatiwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kuimarisha bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na wa kati kwa kuwapatia mafunzo, masoko na mitaji ya kuendeleza biashara zao.

### 1.4.7. Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006)

Sera ya Elimu Zanzibar ipo kwa ajili ya kuhamasisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina zote za maarifa na ujuzi kwa maendeleo ya watu na kuboresha maisha ya jamii. Sera hii pia, inadhamiria kuibadili jamii ya Zanzibar iwe ni mtaji wa rasilimali watu na iweze kupambana na changamoto za kubadili mazingira kiuchumi na kijamii ili kuchangia kwenye mafanikio ya Malengo ya Taifa ya Ukuaji wa Uchumi. Inasisitiza ongezeko la kiushindani, kiujasiriamali na ubora wa nguvukazi utakaosababisha ubora katika uwezo wa kuajiriwa na ambao

umeongeza fursa za kuzalisha kipato. Kupitia ~~s~~Sera ya Elimu ndipo tunapata nguvukazi ambayo inatumika kuajiriwa au kujiajiri. Pamoja na kuwa na ~~Se~~ra ya Uwezeshaji inayolenga watu wote, watu waliopitia katika mikondo ya elimu ndio wengi na ambao ni rahisi kuwajengea uwezo ili waanze shughuli za uzalishaji.

Taasisi za elimu ambazo chini ya miongozo ya sera ya elimu zinatoa elimu za ujuzi na mafunzo ya amali na chanzo muhimu cha kupata Vijana wanaoingia katika mifumo ya uwezeshaji. Mahusiano ya sera hizi mbili pia yapo katika utayarishaji wa mitaala ya elimu ya ujsiriamali ambayo ina lengo la kutoa Vijana wenye ujuzi wa kujiajiri na kuajiri wenzao na kupunguza tatizo la ajira nchini.

### 1.4.8. Sera ya Uhakika wa Chakula na Lishe ya Zanzibar (2008)

Sera hii inasisitiza umuhimu wa uhakika wa chakula katika familia na nchi nzima ambao unategemea sana uwezo wa wananchi kuzalisha au kununua chakula chao kwa mwaka mzima. Kwa hiyo, Sera inatoa usaidizi katika kuongeza uzalishaji na kusarifu mazao ya kilimo na kuongeza wigo wa shughuli za Kiuchumi Mijini na Vijijini ili kupanua wigo wa fursa mbadala wa maisha na maendeleo ya watu. Pia, Sera imeweka umuhimu wa kuwapatia wakulima mikopo ili waweze kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inaelekeza kuwasaidia wananchi wakiwemo wakulima na wafanyabiashara wadogo wadogo mijini na vijijini kwa kuwapatia mafunzo, mitaji na masoko ili kuendeleza shughuli zao za kiuchumi.

### 1.4.9. Sera ya Ajira ya Zanzibar (2009)

Sera ya Ajira inasisitiza utengenezaji wa fursa za upatikanaji wa ujuzi unaotakikana na Ufanisi katika kujiajiri na kuajirika, kuhamasisha upatikanaji sawa wa fursa za Ajira kwa Wanawake na wanaume na pia Ujuzi na Uchangiaji wa rasirimali na kueleza mahitaji ya makundi maalumu kama vile Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Pia, inaelezea kuanzishwa kwa mazingira wezeshi ambayo yatachochea mabadiliko ya uchumi usio rasmi kuelekea uzalishaji rasmi na ushindani wa kibiashara kupitia ajira zenye staha zitakazozalishwa katika mfumo ulio rasmi. Jitihada zote za kuweka Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi zina lengo la kuwajengea uwezo wananchi ili hatimae waweze kujiajiri kwa kufanya shughuli za uzalishaji zenye tija na kupunguza tatizo la ajira na pia kusaidia utekelezaji wa ~~s~~Sera ya Ajira.

### 1.4.10. Sera ya Maendeleo ya Mifugo Zanzibar (2011)

Sera ya Maendeleo ya Mifugo inalenga kuongoza katika utoaji wa huduma za mifugo ili kuongeza kipato cha wafugaji na kusaidia kuleta maendeleo ya jamii ya wafugaji na wananchi kwa jumla. Maendeleo katika sekta ya mifugo yatasaidia kuongeza mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa na ukuaji wa uchumi kwa ujumla.

Katika kuongeza mchango wa sekta ya mifugo katika uchumi, Sera ya Maendeleo ya Mifugo imetilia mkazo kuongeza thamani mazao ya mifugo. Sera hii pia inachochea kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya ndani pamoja na kushajihisha mauzo katika masoko ya ndani na

nje. Itaongeza usaidizi kwa wajasiriamali wa sekta ya mifugo na itahamasisha kuongeza thamani kwa mazao na rasilimali zitokanazo na mifugo.

### 1.4.11. Sera ya Afya ya Zanzibar (2011)

Afya njema ni jambo la msingi na la muhimu sana ili kutekeleza mipango ya kuwawezesha wananchi kiuchumi. Sera ya Afya ya Zanzibar inaeleza haja ya watu wa Zanzibar kupata haki yao ya huduma bora ya Afya itakayotolewa kwa gharama nafuu inayokidhi hali yao. Sera inahimiza matumizi ya mtazamo wa kijinsia na haki za binadamu katika mfumo wa Afya za watu na kuimarisha usafi wa mazingira pamoja na kuondosha uchafu (taka ngumu na za maji maji) zinazotoka katika maeneo ya Afya, sekta za umma na binafsi. Pia, Sera inatilia mkazo juu ya kuimarisha mgawanyo wa mifumo ya usimamizi wa Afya ikiwemo Afya ya Umma, utayari kwenye dharura na kushughulikia. Inawezesha kuzuia, kusimamia na ukarabati wa miundombinu rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu na kuzingatia upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi mengine maalum**.**

### 1.4.12. Sera ya Ushirika ya Zanzibar (2014)

Sekta ya Ushirika Zanzibar kwa sasa inaongezeka umuhimu wake kiuchumi na inachukuliwa kuwa miongoni mwa nguzo muhimu katika kukuza uchumi wa Taifa katika kufanikisha umiliki wa uchumi kwa watu. Sekta hii imefanya kazi kubwa katika kukidhi mahitaji ya watu wake na jamii kwa ujumla na inachangia kupunguza umasikini wa Kipato. Pia imekuwa na umuhimu katika kuongeza fursa za Ajira karibu nusu ya nguvu kazi iliyopo kwa sasa na pia kupanua huduma za utoaji wa kifedha kupitia Vyama vya Ushirika vya kukopa na kuweka maarufu kama SACCOS. Sekta ya Ushirika imeweza pia kuchangia kuongeza ushiriki wa Wanawake katika kufanya maamuzi na umiliki wa Mali. Kiujumla Vyama Vya Ushirika vinasaidia sana kuweka sawa matumizi ya Rasilimali za Umma pamoja na Ukuaji wa Pato la Ndani (GDP).

Uhusiano mkubwa wa kisera kati ya Sera hii na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni kutumia mfumo wa ushirika katika kuwawezesha wananchi kiuchumi. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itawawezesha wananchi kiuchumi kwa kupitia vikundi vya ushirika.

### 1.4.13. Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar (2014)

Sera imejumuisha mifumo ya hifadhi ya jamii ambayo inajumuisha hifadhi ya jamii na misaada kwa jamii. Hifadhi ya jamii ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza na kuondoa umasikini na kuleta usawa katika jamii. Pia, Sera hii inaainisha programu mbali mbali zinazofanywa ili kupunguza makali ya umasikini na athari zitokanazo na majanga na madhara yasiyotegemewa kwa maisha ya watu. Kupitia malengo ya sera hii, program za hifadhi ya jamii zinasaidia kuondoa tafauti kubwa ya kipato kwa wananchi. Sera imeweka utaratibu wa kusaidia makundi maalum yenye uhitaji wakiwemo Wazee. Hivyo, Sera hii ina uhusiano wa moja kwa moja na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa kusaidia makundi hayo yaliyo chini ya hifadhi ya jamii kuendeleza na kuongezea kile wanachokipata kupitia programu ili kiwe endelevu kwa ajili ya maisha yao.

### 1.4.14. Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar (2014)

Maendeleo endelevu yanawalenga watu na miongoni mwao wapo wanaoishi katika Wilaya mbali mbali mijini na vijijini. Sera ya Serikali za Mitaa inasisitiza juu ya kugawanya madaraka katika ngazi za chini ili maendeleo yanayofikiwa yawe endelevu yanayomilikiwa na watu. Watu wenyewe ndio waamuzi wa juu ya nini kifanyike, utekelezaji wa maamuzi, ufuatiliaji na tathmini lazima vihusishe watu wa ngazi za chini kabisa. Kwa maana hiyo sera hii imetilia mkazo ushirikishaji wa wananchi kikamilifu katika maamuzi, kupanga na kutekeleza programu na miradi husika. Moja kati ya misingi mikuu ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni ushirikishaji wa wananchi katika kupanga na kuamua shughuli za kiuchumi zitakazoweza kuwatoa wananchi katika dimbwi la umasikini. Kwa maelekezo ya sera, wananchi katika ngazi za chini kiutawala watawezeshwa katika wilaya zao. Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilitakiwa kutenga sehemu ya mapato yake kwa ajili ya kuwawezesha wananchi ikiwemo Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu. Sera hizi mbili zitafanyakazi kwa mashirikiano ya karibu sana ili kufanikisha malengo ya kuwawezesha wanachi kiuchumi hasa maeneo ya vijijini.

### 1.4.15. Sera ya Jinsia Zanzibar (2016)

Sera ya Jinsia Zanzibar inatafsiri kwa vitendo Mikataba ya Kimataifa na Maazimio ya Kikanda inayotilia mkazo uzingatiaji wa jinsia na kuweka fursa sawa za uwezeshaji wananchi kiuchumi baina ya Wanawake na wanaume. Kuondoa vikwazo na mila potofu zinazowanyima Wanawake na wasichana kumiliki rasilimali na kufaidi fursa zilizopo za kiuchumi. Sera hii inahimiza Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuzingatia uwiano na usawa wa kijinsia.

### 1.4.16. Sera ya Afya Usalama na UsalamaAfya Kazini (2017)

Sera ya Afya na Usalama Kazini inaendana na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa inayohusiana na kusimamia mazingira salama ya kazi na usalama wa watenda kazi nchini. MKUZA unasisitiza haja ya kuwepo kwa miongozo na sera zilizo wazi ambazo zitasimamia waajiri na waajiriwa kufuata taratibu za kazi. Hivyo sera ya Afya na usalama kazini inasimamia shughuli na mambo yote yanayohusiana na kupunguza visababishi vya athari katika mazingira ya kazi, kupunguza gharama ya kutibu majeraha au maradhi yanayotokana na mazingira ya kazi na hatimae kuinua hali ya uzalishaji na kipato kwa ujumla.

Katika harakati za uwezeshaji kiuchumi kupitia ukuzaji wa ujuzi, elimu na taaluma, kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali kuanzia upatikanaji wa mali ghafi, uzalishaji, masoko pamoja na usimamizi wa miradi hiyo unahitaji muongozo kwa ajili ya kuweka usalama na kuzingatia afya ya watendaji ambapo sera hii inafanya kazi hiyo. Hivyo mahusiano kati ya sera ya Usalama na Afya kazini inaenda sambamba na uwekaji wa mazingira bora ya kazi katika Nyanja zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi hapa Zanzibar.

### 1.4.17. Sera ya Taifa ya Ardhi Zanzibar (2018)

Ardhi ni moja kati ya maeneo yaliyopewa kipaumbele tangu miaka ya mwanzo baada ya Mapinduzi. Hatua ya kuwagaia wananchi eka tatu ilkuwa na lengo kwanza kuwawezesha ili

wazalishe na wajitegemee kiuchumi, lakini pia kusaidia kuweka hali za wananchi sawa. Sera ya Ardhi inasimamia haki ya upatikanaji wa Ardhi, matumizi bora na usimamizi wake kwa ajili ya maendeleo kuelekea kuondoa umasikini kama ilivyodhamiriwa kufikiwa na Dira ya Zanzibar 2050. Ardhi inatakiwa ionekane kama mtaji wa kuongeza utajiri na mafanikio ya Kiuchumi. Mazingatio ya kupata ardhi hapa Zanzibar ni katika hali ya usawa kwa Wanawake, Wanaume na makundi yote kwa njia ya kupewa baada ya kuomba, kurithi, zawadi, kununua na utambuzi wa haki kupitia taratibu za kisheria. Kwa kuwa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inahimiza wananchi kufanya shughuli mbali mbali za maendeleo, ardhi hutumika kama nyezo kuu ya kufikia malengo hayo. Ardhi inatumika kama mtaji au dhamana ya kupata mtaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi.

### 1.4.18. Sera ya Utalii Zanzibar (2018)

Kiasi kikubwa cha fedha za kigeni kinatokana na Utalii. Sera ya Utalii ya Zanzibar inatambua umuhimu wa kutoa huduma bora ili kuvutia wageni wanaotembelea visiwa vya Zanzibar. Kwa hivyo inasisitiza wadau wa utalii lazima wawe wabunifu na wawe tayari kupokea na kutumia teknolojia za kisasa na zilizo rahisi katika kufanya kazi zao ili kukidhi matarajio ya wateja katika njia mbali mbali. Sekta ya Utalii ya Zanzibar ni mchanganyiko wa vivutio vya asili, utamaduni na urithi uliotapakaa Zanzibar, uliochanganyika na huduma mbalimbali zinazotolewa na wadau wadogo wadogo na wa kati wa sekta ya Utalii (SMEs). Mbali na kuvutia wageni, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ina mahusiano ya karibu na sera hii ya utalii, kwa upande wa wananchi ambao wanahitaji kunufaika na sekta hiyo, zamani bidhaa mbali mbali zilizokuwa zina~~zo~~tumika mahotelini zilikuwa zikinatoka nje ya Zanzibar, hali hiyo imekuwa ikipungua hatua kwa hatua, kutokana na kwamba wananchi wa Zanzibar wanazalisha bidhaa hizo. Jambo hili linawezekana kwa jitihada kubwa za kuwawezesha wananchi ili kuweza kuzalisha kwa kiwango bora na kupata soko mahotelini.

### 1.4.19. Sera ya Michezo ya Zanzibar (2018).

Michezo ina umuhimu mkubwa katika Maendeleo ya Jamii. Hii inatokana na mapato ya wachezaji, vilabu na kodi inayokusanywa katika viwanja vya michezo na wakati mwingine hutumika kama kiungo muhimu cha kuleta Amani na Utengamano baina ya Mataifa. Michezo Zanzibar husaidia kujenga umoja na mshikamano, kujenga afya ya jamii na kujenga uchumi, ajira pamoja na kuleta mashirikiano baina ya jamii mbali mbali. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatambua umuhimu wa michezo kwa kuweka Wizara inayoshughulikia maendeleo ya michezo, Baraza la Taifa la Michezo pamoja na kuimarisha michezo kwenye skuli na vyuo kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kupitia Wizara inayoshughulikia Michezo na Taasisi binafsi za michezo, Serikali inachukua jitihada nyingi kutatua changamoto mbali mbali za michezo katika uendeshaji wa michezo, vyama vya michezo, miundo mbinu, sera na sheria za michezo kwa maslahi ya michezo na wanamichezo. Michezo ni nyenzo muhimu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwani kuna fursa nyingi za ajira hasa kwa Vijana.

### 1.4.20. Sera ya Diaspora Zanzibar (2018)

Sera ya Diaspora Zanzibar inathamini wanadiaspora wenye asili ya Zanzibar katika kuleta Maendeleo ya Kiuchumi na Kijamii ya Zanzibar. Uwepo wa Sera hii kutasaidia kutafuta na kuelekeza matumizi sahihi ya fursa mbalimbali zitakazosaidia katika kuharakisha Maendeleo ya Zanzibar. Fursa hizo ni pamoja na misaada ya kifedha inayotolewa na Wanadiaspora kwa jamaa zao, uwekezaji, taaluma, ujuzi na teknolojia. Hivyo, Sera hii inatoa muongozo kuhusu namna wanadiaspora wa Zanzibar watakavyoshiriki katika kuleta Maendeleo ya Nchi yao ya asili kupitia fursa na misaada mbalimbali ambayo itasaidia kuwawezesha Wananchi wa Zanzibar kukuza elimu na taaluma zao, kukuza uwezo wa kubuni, kuanzisha na kutekeleza miradi mbali mbali ya Kiuchumi na kijamii pamoja na kuinua kipato chao na cha Taifa kwa ujumla.

### 1.4.21. Sera ya Watu Wenye Ulemavu (2018)

Sera hii inaweka mkazo wa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu na ushiriki kamilifu wa watu wenye ulemavu katika shughuli na programu zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sera imeweka mkakati wa kuhamasisha wadau kuweka miundombinu wezeshi katika programu zote za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili Watu wenye Ulemavu kuweza kunufaika na kufaidika na fursa hizo.

### 1.4.22. Sera ya Viwanda ya Zanzibar (2019)

Sera ya Viwanda ya Zanzibar ni moja kati ya Sera za Serikali ambazo zimeweka kipaumbele kwenye maendeleo ya Biashara ndogo na za kati. Sera ya Viwanda kwa uwazi kabisa inaelezea Sekta ndogo ya biashara kama chachu ya maendeleo na inatoa mikakati ya kuiinua Sekta binafsi, ikiwemo kupitia ubinafsishaji wa biashara zinazomilikiwa na Serikali. Sera imesisitiza kuinuliwa kwa viwanda vya kusafirisha biashara Nje na viwanda vidogo vidogo vya ndani, wakati huo huo kusaidia viwanda ambavyo ni visaidizi. Kwa hiyo, Sera hii imelenga kusaidia sekta zisizo rasmi kuwa Sekta rasmi na maendeleo yake kama kitovu cha kulea na kukuza ujasiriamali na ukuaji wa biashara. Sera inatilia mkazo kwenye biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs), kuzalisha utajiri na kutengeneza Ajira. Sera ya Maendeleo ya Viwanda inasisitiza juu ya biashara ndogo ndogo na za kati (MSMEs) kutengeneza vipato na Ajira. Sera hii imeweka mikakati ya kuweka maeneo ya kuanzisha viwanda kila eneo na kuwasaidia wajasiriamali wa kati kupata mitaji na mafunzo ya kuanzisha viwanda hivyo. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inauhusiano wa karibu sana na Sera hii katika kuwasaidia wajasiriamali wachanga na hata wa kati kuendeleza uzalishaji, kuwapatia nyenzo za uzalishaji na hatimae kuanzisha viwanda vidogo vidogo.

### 1.4.23. Sera ya Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo Wadogo (2019)

Sera ya Fedha kwa wajasiriamali wadogo wadogo imeweka mkazo katika utoaji wa huduma za kifedha ili zipatikane kwa watu wengi wa Zanzibar kwa lengo la kuimarisha ukuaji wa uchumi. Sera hii ina mahusiano na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kuweka mikakati mbali mbali ya kuleta maendeleo endelevu kwa sekta ndogo ndogo za fedha kwa wananchi.

### 1.4.24. Sera ya Uchumi wa Buluu (2022)

Zanzibar ni Nchi ya visiwa vilivyozungukwa na bahari na ina eneo kubwa la bahari na maliasili nyingi za mwambao na baharini ambazo hazijatumika ipasavyo. Wananchi wengi wa Zanzibar wanajishughulisha na sekta tofauti za uchumi wa buluu kama njia ya kujipatia kipato. Sekta ya Uchumi wa Buluu ni mtambuka na inashirikisha Sekta nyingi zikiwemo, uvuvi, utalii, kilimo cha mwani, mafuta na gesi, michezo ya baharini na ufukweni pamoja na sekta ya usafiri wa baharini. Hali hii imesababisha Serikali kuandaa sera na programu mbali mbali na kuweka kipaumbele katika kushughulikia uchumi wa buluu. Sera ya Uchumi wa Buluu imeweka muongozo wa kuwawezesha wananchi kiuchumi utakaosaidia kujiajiri na kuajiriwa katika sekta hizo. Kuna fursa nyingi za kiuchumi katika sekta za uchumi wa buluu hivyo, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itawasaidia wananchi kuzitambua fursa zilizopo katika uchumi wa buluu na namna ya kutumia fursa hizo katika maeneo yao. Ili lengo hilo liweze kutimia, Sera hiyo itasaidia kuwaandaa wananchi kuingia katika sekta hiyo kwa ufanisi kwa kuwawezesha kwa mafunzo, mitaji na masoko ya bidhaa na huduma katika sekta za uchumi wa buluu.

Vile vile, kuna fursa kubwa kwa makampuni ya nje ya nchi kuwekeza katika sekta za uchumi wa buluu, Hivyo, ni muhimu kwa wananchi wa Zanzibar kuzitumia fursa ya kuwepo kwa makampuni hayo kuwekeza na kuunganisha miradi yao midogo midogo na huduma katika makampuni hayo yatakayowekeza. Wananchi hao wanahitaji kuwezeshwa ili ushiriki wao uwe wa ufanisi na wenye tija katika kuwekeza na kuzitumia fursa.

Sera zote hizo zina uwiano wa karibu na utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na zina mahusiano ya karibu pamoja na kuchochea utekelezaji mzuri wa Sera hii. Sera hizi zinaeneza uchocheaji wa tija kwa taifa wa kukuza kipato cha mwananchi, kukuza uchumi, kupata wazalishaji wenye tija na kuzalisha ajira kupitia ujasiriamali na uwezeshaji kwa Vijana, Wanawake, Watu wenye Ulemavu na jamii kwa ujumla.

# SURA YA PILI

## 2.0 HALI HALISI

Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni ishara ya jumla ya maendeleo endelevu ya Kiuchumi na kijamii. Neno uwezeshaji lina maana ya uwezo wa kufanya jambo kwa vigezo na ubora unaotakiwa. Shughuli za Uwezeshaji wananchi Kiuchumi zina maana ya kujenga fursa kwa matumizi ya rasilimali za ndani katika namna yenye tija na ufanisi. Uwezeshaji wananchi kiuchumi ni pamoja na kutoa ujuzi, huduma na fursa kwa wazawa na jamii ya watu masikini zinazotaka kuendelea kiuchumi.

Tangu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilipoanza hapa Zanzibar zililenga zaidi kuondoa umasikini ndani ya jamii, hii ilitokana na tafiti zilizoonesha kuwepo kwa idadi kubwa ya watu masikini. Awali, mkazo mkubwa ulielekezwa kuwapatia wananchi huduma muhimu za kijamii zikiwemo huduma za afya, elimu na maji. Baadae haja ya kuwapatia wananchi uwezo wa kuongeza kipato ikajitokeza na ndipo dhana ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ikaibuliwa.

### 2.1 Muktadha wa Kijamii na Kiuchumi

Zaidi ya miaka kumi iliyopita, Zanzibar imeweza kuendeleza na kuenzi mafanikio makubwa ya uchumi, ikiwa ni pamoja na ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa kiwango cha asilimia 7 katika mwaka 2019 (Zanzibar Statistical Abstract 2019). Uchumi wa Zanzibar unategemea sana sekta kuu tatu, ambazo ni kilimo, viwanda na huduma (Utalii). Mwaka 2020, Huduma ilikuwa ni Sekta iliyoongoza ambayo ilichangia asilimia 43.9 ya Pato la Taifa, Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 27.6 na Sekta ya Viwanda ilichangia asilimia 19.3 (Zanzibar Statistical Abstract 2020). Utalii umeongezeka kwa kasi ya ukuaji katika kipindi cha miaka michache iliyopita kwa kuchangiwa na juhudi za Sekta binafsi. Zanzibar imefikia Uchumi wa Kati Daraja la chini mwaka 2020.

Kipato cha mtu mmoja mmoja kimepanda kutoka Shilingi za Kitanzania TSh 1,806,000 katika mwaka 2016 na kufikia Shilingi za Kitanzania TSh 2,549,000 kwa mwaka 2019. Pia, ongezeko hilo limeonekana kwa upande wa Dola ya Kimarekani ambapo pato la mwananchi limepanda kutoka Dola za Kimarekani 830 kwa mwaka 2015 na kufikia Dola 1,114 katika mwaka 2019. Ingawa Uchumi wa Zanzibar unakuwa, lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahitaji kuhakikisha kuwa Wazanzibari wengi wananufaika kisawasawa na ukuaji huu. Idadi ya Watu wanaoishi chini ya mstari wa Umasikini ni asilimia 9.3 (Zanzibar Vision 2050).

Katika kupambana na changamoto hizi, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imebadilisha biashara na uwekezaji tangu 1985 na kubinafsisha uchumi wake lakini watu wake bado hawajaitumia fursa hii kikamilifu. Kukosekana kwa njia inayoeleweka katika uwepo wa Fedha, mifumo isiyojitosheleza kama vituo vya kukuza teknolojia, huduma za Maendeleo ya

Biashara pamoja na kutopatikana kwa Sekta muhimu kwa ajili ya masikini na ukuaji ni miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta hii.

### 2.1.1. Miundo mbinu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lengo lake ni kutoa huduma kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha na kuendeleza biashara na miradi mbalimbali ya maendeleo. Vituo hivi hutoa huduma katika maeneo makuu matatu ikiwemo, huduma za elimu ujuzi wa aina mbali mbali, huduma za masoko kwa bidhaa za wajasiriamali na baadhi ya vituo vinakuwa na utaratibu wa kutoa huduma za mitaji. Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi vilivyopo Zanzibar ni pamoja na Vituo vya mafunzo ya amali ambavyo vinaendeshwa na Serikali na vyengine ni vya binafsi na Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali kimoja tu ambacho ni kituo cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vituo vya mafunzo ya amali vimeanzishwa kwa matakwa ya kisheria iliyoanzisha Mamlaka ya mafunzo ya amali Zanzibar. Pamoja na kutoa mafunzo ya amali, Mamlaka ya mafunzo ya amali imepewa jukumu la kusimamia vituo vyote vya mafunzo ya amali vya Binafsi vilivyopo Zanzibar. Walengwa wa vituo hivi ni Vijana waliomaliza katika mfumo wa elimu kuanzia darasa la kumi. Jumla ya vituo 4 vya serikali na 40 za binafsi ambavyo vinatoa jumla ya fani 16. Changamoto kubwa katika vituo hivi vya mafunzo ya amali ni uhaba wa fani, vifaa, maeneo ya kufanyia kazi za vitendo na walimu.

Mbali na Vituo vya Mafunzo ya Amali, Vile vile, kuna Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali Zanzibar kilichoanzishwa mwaka 2015. Kwa sasa kipo kimoja tu ila Serikali inaendelea na maandalizi ya kujenga kituo kingine Unguja na Pemba kitakachokidhi mahitaji ya utoaji wa huduma mbali mbali za Ujasiriamali kinadharia na kivitendo. Walengwa wa kituo hiki ni wananchi wote ingawa kwa kiasi kikubwa wanaojiunga na kituo ni Vijana na asilimia 86 ni Wanawake. Kituo hiki kilianzishwa kutokana na mapendekezo ya utafiti uliofanywa kuiangalia hali ya ujasiriamali na changamoto za wajasiriamali zilizopo hapa Zanzibar. Utafiti ulipendekeza kuanzisha kituo cha kitaifa Unguja na tawi lake kwa upande wa Pemba.

Kuna Kituo kimoja kinachotoa mafunzo yanayohusiana na kutengeneza vifaa vya umeme wa Jua kwa kina mama. Aidha, Kituo hiki kinatoa mafunzo ya ushonaji na ufugaji wa nyuki.

Pia, utafiti ulipendekeza kuanzishwa vituo kama hivyo katika kila Taasisi ya elimu ya juu ili kuwaunganisha Vijana wanaomaliza katika fani mbali mbali kuanza kuzitumia fani walizosomea za ujasiriamali na kujiajiri kabla ya kufikiria kuajiriwa. Katika kituo hiki Vijana wanaojiunga wanatakiwa wawe na mawazo ya biashara au biashara ndogo walizozianzisha wanalelewa kwa kukuza biashara zao mpaka kufikia hatua ya kusajili na kuanzisha kampuni ndogo ndogo ili kuendesha biashara zao. Hadi kufikia Agosti 2021, jumla ya Wajasiriamali 1,500 (1,170 Wanawake na 330 ni wanaume) wamepatiwa mafunzo ya Usarifu wa Bidhaa na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na jumla ya Kampuni 80 zenye Vijana kati ya 2 hadi 5 zimeundwa.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kituo hiki kinakabiliwa na changamoto za uhaba wa nafasi kwa ajili ya mafunzo ya nadharia na vitendo. Pia, kuna uhaba wa wataalamu wa kuandaa programu na kufundisha taaluma mbali mbali zinazokwenda sambamba na soko la ajira nchini. Kituo kinahitajika kuwa na maeneo ya kufanyia kazi kwa vitendo na mazoezi kwa fani mbali mbali, kwa sasa mazoezi ya fani zote yanafanywa katika eneo moja jambo ambalo ni kinyume kitaaluma. Isitoshe Vijana wanaomaliza muda wao wa kulelewa wanabaki na kuendelea kufanya biashara zao katika kituo kwa sababu wanakosa maeneo ya kufanyia biashara zao, jambo hili linawanyima nafasi Vijana wengine kujiunga na kituo.

Mbali na kuwa na utaratibu wa kuwapatia na kuwaunganisha na fursa za mikopo, Vijana wanaomaliza katika vituo hivi wanakosa vifaa kwa ajili ya kufanya kazi walizojifunza. Mara nyingi vifaa vinavyohitajika kuanzisha kampuni au Taasisi kwa ajili ya kujiajiri vinahitaji pesa nyingi ambazo Vijana hao hawamiliki na Serikali inakuwa na uwezo mdogo wa kulishughulikia eneo hili.

Changamoto nyingine ni ukosefu wa vifaa vya kuanzia biashara, ilitakiwa wanapomaliza muda wa kulelewa Vijana hao wapatiwe nyenzo kwa mujibu wa biashara wanazofanya. Hili limekuwa ni tatizo na ndio maana wengi wanataka kubaki kituoni ili waendelee kutumia mashine na huduma za kituoni hapo. Wakati mwengine inajitokeza Vijana wanakuja na ubunifu wa teknolojia inayohitaji kuendelezwa lakini inashindikana kwa kukosa utaalamu na vifaa husika ambavyo ni ghali.

Vituo vya Huduma za Biashara na Ujasiriamali (EBDS) navyo ni muhimu katika kuwawezesha Wananchi Kiuchumi. Kwa bahati mbaya hatuna vituo vya aina hiyo hasa kwa wajasiriamali, lakini kutokana na umuhimu wake, Wizara inayohusika na masuala ya uwezeshaji imeanzisha madawati ya kutoa huduma za biashara kwa wajasiriamali katika Wilaya za Unguja na Pemba, na huduma zinazotolewa kwa sasa ni huduma za mafunzo. Ili huduma hizi ziweze kupatikana ipasavyo kunahitajika jengo ambalo litakuwa na Afisi moja na maeneo ya kutolea huduma zote muhimu za wajasiriamali.

Mfumo wa barabara na mawasiliano Zanzibar umeunganisha maeneo tofauti ambapo imeweza kuimarisha masoko kwa bidhaa za wajasiriamali. Barabara za ndani kuelekea maeneo ya uzalishaji na maeneo ya utalii bado zipo kwenye hali mbaya, ukiongezea na umbali mrefu kwa ujumla ni kero kwa usafiri kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo pamoja na usafirishaji wa mazao. Barabara za ndani kuelekea vijijini na maeneo ya uzalishaji ni mbovu na maeneo mengine hazipitiki hivyo kuleta usumbufu wa ufikiwaji na kuzorotesha uzalishaji kutokana na ugumu wa kufikika. Pia, Hali hii inazorotesha shughuli za uwekezaji kutokana na kukosekana kwa miundombinu muhimu hasa katika maeneo ya vijijini.

Vile vile, Vijana wanahitaji kuwa na vituo ambavyo vitakua ni vitovu vya mafunzo kwa ~~ya~~ Vijana kiwilaya vitakavyotumika kutoa mafunzo ya aina mbali mbali ya kukuza ustawi na maendeleo ya Vijana pamoja na kuwapatia habari na fursa mbali mbali zikiwemo za ajira na fursa nyengine za kiuchumi na kijamii. Huduma za kijamii ni moja wapo ya miundombinu inayohitajika katika shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Huduma za maji, barabara,

umeme na mawasiliano zimefikishwa katika maeneo mengi ya mjini na vijijini. Miundombinu ya maji na umeme mbali na kutumika kama huduma pia ni nyenzo muhimu sana kwa uzalishaji katika sekta zote hasa katika kuwawezesha wananchi. Hata hivyo, baadhi ya miundombinu hiyo imechakaa kwa kiasi kikubwa na kusababisha upatikanaji wa huduma hizi muhimu kuwa dhaifu na usiokidhi mahitaji. Ukosefu wa umeme wa uhakika unaendelea kuwa ni kikwazo katika ukuaji wa Uchumi na ushindani wa biashara hasa katika baadhi ya viwanda na wajasiriamali. Aidha, huduma katika sekta ya utalii nazo zinaathiriwa na umeme usiokuwa wa uhakika.

Huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ni muhimu sana katika kuwaunganisha Wajasiriamali na Wafanyabiashara. Kutokuwepo na uhakika wa huduma hizi hasa vijijini kunawakosesha fursa wazalishaji kupata habari na taaluma sahihi za mafunzo kwa kuimarisha uzalishaji na masoko ya bidhaa zao. Vile vile inawanyima fursa ya kutumia teknolojia katika shughuli mbali mbali za ujasiriamali katika sekta ya fedha na utafutaji wa masoko ya bidhaa zao.

### 2.2. Mafunzo ya Uwezeshaji.

Mafunzo ya Uwezeshaji yanalenga kuwawezesha Wananchi Kiuchumi kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo husika ili waweze kujiajiri na kuajiri wengine, kupunguza umasikini na kuchangia kukua kwa uchumi. Wananchi wengi wanakwama kwenye shughuli zao za uzalishaji kutokana na kukosa elimu sahihi ya ujasiriamali/ biashara ambayo itaimarisha uzalishaji. Zanzibar bado haijaandaa Mtaala au Mfumo mzuri wa Kitaifa wa kuwafundisha wajasiriamali ambao utalenga kuimarisha shughuli wanazozifanya. Watoaji wa mafunzo ya ujasiriamali na biashara huandaa mitaala yao kulingana na uwezo na uzoefu wao na si kwa mujibu wa matakwa halisi ya wajasiriamali na soko la ajira. Mafunzo ya aina hii, hayawaongezei ujuzi wajasiriamali na hubaki na usimamizi mbaya wa miradi na biashara zao, kwa wale wazalishaji huendelea kuzalisha bidhaa hafifu na dhaifu na matokeo yake hukosa soko. Vile vile, changamoto kubwa ni kwamba mafunzo machache yanayopatikana hutolewa katika maeneo ya mijini tena kwa gharama kubwa.

Wengi hawana elimu ya kutosha ya usimamizi wa miradi, fedha, mbinu za masoko au hata biashara. Hii ni changamoto kubwa kwani hata yale mafunzo machache yanayopatikana hutolewa maeneo ya mijini tena kwa gharama kubwa ambayo wananchi wengi hawamudu. Pia, katika suala la mafunzo kunakosekana ubunifu na Taasisi nyingi zinatoa aina moja ya mafunzo na zinakosa uwezo wa kutumia fursa zilizopo nchini na kuandaa mafunzo yatakayoweza kuzitumia fursa hizo kikamifu katika uzalishaji. Eneo la mnyororo wa thamani na ubunifu bado ni eneo hafifu na halijafanyiwa kazi ipasavyo na ufadhili katika eneo hili ni mdogo. Vifaa vya Ufundishaji wa shughuli mbali mbali hasa za usarifu ni ghali na hakuna motisha za kuwasaidia wajasiriamali. Ni sekta chache ambazo zinatoa mafunzo ya kuongeza mnyororo wa thamani. Kwa kipindi cha miaka 5 kuanzia (2015 – 2020) wanufaika waliopata mafunzo katika Kituo cha Kulea na Kukuza Ujasiriamali Zanzibar (ZTBI) wamefikia 1,197 ambao Wanawake ni 924 na wanaume ni 273 kwa mazao ya kilimo na mifugo (ZTBI Report 2020).

Mafunzo ya uwezeshaji hutolewa kwa njia mbili kuu; mafunzo ya nadharia na mafunzo ya vitendo. Mafunzo ya nadharia yanahusisha Ujasiriamali, nadharia ya biashara, mipango ya biashara usimamizi wa fedha za mradi au biashara, masoko, utafutaji wa mitaji na mafunzo mengine ya nadharia huandaliwa kulingana na mahitaji ya wajasiriamali wa eneo husika.

Kwa kuwa ujasiriamali na shughuli za uwezeshaji kwa ujumla ni vitendo zaidi, mambo yote yanayofundishwa kwa nadharia hufundishwa kwa vitendo. Kwa hivyo, mafunzo ya vitendo yanajumuisha uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa lengo la kumuwezesha mlengwa kufanya biashara aliyoisomea na kujiajiri. Kuna changamoto kwa wajasiriamali wengi kufanya biashara ambazo hawana ujuzi nazo na ~~hivyo~~ kusababisha changamoto nyingi wakati wa kufanya biashara zao hatimae biashara hizo zinashindwa kuendelea. Pia, wajasiriamali hukosa ubunifu na mara nyingi huiga biashara ya mwengine bila ya kufanya ubunifu wa kuiboresha zaidi.

Taasisi za Serikali na Taasisi zisizokuwa za kiserikali zinatoa mafunzo ya uwezeshaji katika sekta mbali mbali. Hata hivyo, Taasisi nyingi hutoa mafunzo ya nadharia zaidi kuliko vitendo, jambo ambalo halisaidii sana wajasiriamali. Aidha, mafunzo yanayotolewa yanakosa uratibu mzuri, kiasi kwamba huishia kuwafunza wananchi hao hao kila mara na ndio maana wajasiriamali wengi hubaki na malalamiko kuwa hawajapatiwa mafunzo. Isitoshe kila Taasisi hutoa mafunzo kwa namna yake na ubora wake jambo ambalo husababisha kujenga ujuzi na uelewa tafauti wa wajasiriamali katika fani moja. Hali hii husababisha kutengeneza bidha aina moja yenye kiwango tafauti na hapo tena hujitokeza matatizo ya soko.

#### 2.2.1. Fikra Mgando

Utafiti mdogo juu ya ujasiriamali 2012 umefichua kwamba, Vijana wengi wana mawazo mgando ya kuona na kutaka kuajiriwa katika Taasisi rasmi hasa za kiserikali. Hii ilikuwa inaweka kikwazo na mkwamo katika maendeleo ya ujasiriamali kwa Zanzibar. Mabadiliko ya kifikra yanahitajika kwa ajili ya kujenga utayari kwa mtu na hatimae kuleta Ajira binafsi na uwezekano wa kuajiriwa, kuongeza ubora na wingi wa mazao ya Sekta za wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs), uwezeshaji kwa Vijana na makundi maalum na maendeleo endelevu kwa Zanzibar. Kubadili fikra mgando hakukuchukuliwa kama jambo muhimu katika uwezeshaji kiuchumi na maendeleo ya ujasiriamali.

Dhana tatu zinatakiwa kubadilika ili watu wafanikiwe na kuwa na dhana sahihi ya Uwezeshaji Kiuchumi (fikra sahihi, uelewa au matumizi ya akili), Sifa (Itikadi) na Msimamo. Mabadiliko ya fikra yanatakiwa kujumuishwa katika maeneo au masuala yote ya Kiuchumi ili kuwe na matokeo chanya kwenye kupunguza na kuondoa umasikini.

Changamoto kubwa katika mabadiliko ya fikra yanahitaji muda wa ziada na jitihada madhubuti. Kupitia mchakato huu, sio tu watu ~~sio tu~~ watakuwa na dira lakini pia kuisimamia na kujitoa muhanga kwenye kuitimiza dira hiyo. Kwa hiyo, matendo madhubuti ambayo yatazalisha ubora unaoonekana kwa kujenga hamasa ya kujitegemea yanahitajika sana. Ndio maana mabadiliko ya fikra na mienendo miongoni mwa watu wa Zanzibar ni muhimu kwa uwezeshaji kiuchumi na maendeleo ya kijamii.

### 2.2.2. Utamaduni wa Ujasiriamali na Uwezo

Utamaduni wa kijasiriamali ni mchakato ambao unaweka thamani ya Taasisi kwa waanzilishi wake. Unaleta muingiliano na uelewa kwa waajiriwa wapya jinsi ya kuwahudumia wateja wao, wanavyojichukulia wao wenyewe, wanavyofanya kazi zao na kwa ujumla namna ya kufanikiwa ndani ya biashara.

Kwa mujibu wa Makadirio ya Idadi ya watu ya mwaka 2021, Vijana wengi wa kike na kiume Zanzibar (asilimia 35.4) hawana utamaduni wa kiujasiriamali ndio maana hawawezi kubadilisha mawazo, fikra na nguvu zao kuelekea kwenye fursa za kibiashara kwa kutengeneza Ajira binafsi na kujiongezea kipato. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara inayohusika na masuala ya Uwezeshaji imeanzisha kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali huko Mbweni Unguja mwaka 2016 ili kuamsha Vijana kuwa na ari na utamaduni wa kijasiriamali ili waweze kujiajiri wao wenyewe.

Utamaduni na uwezo wa kijasiriamali una nafasi kubwa sana katika mbinu zote za kijasiriamali kama vile kuingia katika masoko na kufanikiwa kwa biashara mpya. Zitatoa mwelekeo wa kutambua fursa, kufanya biashara mpya, kuendesha ubunifu mbalimbali na kujifunza kutoka kwa wengine na kuyafanyia kazi ili kubadilisha mazingira ya hali zao.

Ukubwa wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kulingana na uwezo na utamaduni wa kijasiriamali ni jinsi gani mbinu za kijasiriamali zinafundishwa kwa umakini wa hali ya juu kuhamasisha uvumbuzi wa kijasiriamali kupitia biashara, mbinu za kijasiriamali na uzoefu. Kituo cha Kulea na Kukuza Wajasiriamali cha Zanzibar kimeanzisha mashindano ya mawazo ya biashara ambapo Vijana wahitimu wa Vyuo Vikuu wanahimizwa kuanzisha biashara zao kwa kuandika mawazo yao na washindi watatu wa Mwanzo wanapewa fedha za mtaji pamoja na mafunzo ya kuanza biashara zao.

### 2.2.3. Muundo wa kusaidia Kukuza Biashara

Suala la muundo wa kusaidia kukuza biashara ni ajenda ya uwiano wa kijinsia na ni muhimu katika kuelekea kwenye kusaidia kukuwa kwa Sekta inayoruhusu Wanawake wengi na wanaume kushiriki katika biashara na kufanya mambo kiujasiriamali. Pia, kuna gharama na athari nyingi katika kuingia kwenye masoko ya ajira, ardhi, bidhaa na fedha. Hivyo,
uwepo wa Mifumo saidizi inayotoa ulinzi wa kiuchumi (kupitia hifadhi ya jamii, bima au ugawaji wa mali) kuwezesha watu masikini kuingia katika biashara kwa gharama ya chini na kukua na kuondoa umasikini kwa haraka.

Kuna biashara ndogo ndogo mbali mbali Zanzibar, nyingi zao ni kwenye sekta zisizo rasmi na zisizo na uhakika , ambazo zinahitaji mfumo saidizi ulio sahihi na unaoweza kumudu matakwa ya jamii hiyo kutoka Serikalini na Sekta binafsi kama vile vituo vya kukuza biashara na vile vya kutoa huduma za maendeleo ya Biashara (BDSs). Kuna Kituo cha kulea na kukuza wajasiriamali ambacho kinahudumia Unguja na Pemba, kuna vituo vya huduma za maendeleo ya Uwezeshaji wa Biashara (EBDS) vilivyoanzishwa katika Wilaya ya Kati Unguja pamoja na vituo viwili vya kutoa mafunzo ya uzalishaji wa bidhaa za viwandani Unguja na Pemba. Vyote vipo katika hatua za awali vikiwa na watumishi wachache wenye sifa na uchache wa vifaa kuendana na mahitaji ya ukuaji wa soko.

Ili kuweka mfumo wa utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali/biashara, Wizara inayoratibu masuala ya uwezeshaji imetayarisha kitini kwa ajili ya kufundishia wajasiriamali wa ngazi tofauti. Kitini hiki kina lengo la kudhibiti usawa na uwiano wa ubora katika mafunzo hayo.
Mbali ya changamoto zilizotajwa hapo awali, pia kuna changamoto kwa ujumla wake juu ya mafunzo yanayohusiana na Uwezeshaji. Miongoni mwa changamoto hizo ni: Taasisi kushindwa kuwahudumia walengwa ipasavyo ambapo kumekuwa na wananchi wengi wanaohitaji mikopo, mafunzo na masoko ya bidhaa lakini uwezo wa Taasisi hizo ni mdogo kuliko mahitaji pamoja na kutokuwepo kwa mfumo unaounganisha taarifa za walengwa wa kila Taasisi hali ambayo husababisha Taasisi hizo kutoa huduma za aina moja (mfano mkopo au mafunzo) kwa walengwa hao hao na kuwaacha wengine wanaohitaji huduma hizo.

## 2.3. Upatikanaji wa Masoko

Maendeleo ya shughuli zote za biashara zinataka masoko hata kama huduma itatolewa kwa wingi lakini soko la kuuza bidhaa hizo likikosekana uzalishaji wa bidhaa hizo hautokuwa na maana. Kwa bahati mbaya wajasiriamali wengi pamoja na kuongeza wingi na ubora wa mazao wanayozalisha lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi. Mfano halisi unaonekana katika ongezeko kubwa la uzalishaji wa mazao ya matunda na mboga mboga zinazozalishwa Zanzibar ambapo unapofika msimu yanakosa soko na kupelekea kuuzwa kwa bei ya chini sana. Hii pia inachangiwa na kutokuwepo kwa viwanda vya kusarifu au kuchakata mazao hayo na kuyaongeza thamani.

Jitihada kubwa zaidi zinahitaji kuelekezwa katika utoaji wa elimu ya masoko ili kuongeza thamani na ubora wa bidhaa, ujuzi na taaluma jinsi ya kutafuta masoko ya bidhaa na kufanya uchambuzi wa hali ya masoko ili kujua bidhaa gani na wakati gani wa kuzalisha, walengwa au wahitaji wa bidhaa hizo pamoja na bei itakayopelekea bidhaa zote kuuzika. Jitihada hizo zinakwenda sambamba na masoko na elimu ya masoko na kuwa na maeneo ambayo yatatumika kwa ajili ya kuuzia bidhaa zinazozalishwa. Pia, katika kufanya tafiti za kuangalia bidhaa zenye soko ndani na nje ya nchi.

Masoko ni eneo lenye changamoto kubwa katika Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Wajasiriamali huzalisha bidhaa mbali mbali lakini hawafikii malengo kama inavyokusudiwa kwa kukosa soko, jambo hili limekuwa likiwarejesha nyuma kimaendeleo. Wajasiriamali wengi Zanzibar wanatumia masoko yaliyopo kwa njia za kienyeji, yaani wanazalisha bidhaa zao na kupeleka sokoni kama kubahatisha mteja yeyote atakayempata na bei yoyote ile, utaratibu huu umekuwa na changamoto nyingi na unawavunja moyo wajasiriamali wengi. Taasisi ya kusimamia masoko nchini inahitaji kuimarishwa na kujengewa uwezo ili kuweza kusimamia na kubuni njia mbali mbali za kuhakikisha bidhaa za Wajasiriamali zina masoko ya kutosha.

Hakuna tafiti za kutosha kuangalia ni namna gani tunaweza kutumia malighafi zilizopo nchini kuhakikisha kunakuwepo na masoko ya kutosha kwa bidhaa zinazozalishwa. Na zile bidhaa zenye soko wajasiriamali wanakosa ujuzi wa kuweza kuzalisha kwa kiwango na ubora unaohitajika na soko. Elimu ya masoko ni suala la kupewa kipaumbele kikubwa katika

kuimarisha uzalishaji kwa wajasiriamali. Aidha, ubunifu katika utoaji huduma mbali mbali kwa kupitia mtandao ikiwemo kusambaza bidhaa kwa wateja bado haijazingatiwa ipasavyo kwa kiasi gani inasaidia watoa huduma kupata soko la uhakika na wateja kusogezewa huduma hizo kwa karibu zaidi. Hivyo, Sera hii iangalie ni namna gani inaweza kuwasaidia wajasiriamali kutumia ubunifu na teknolojia katika kukuza masoko ya bidhaa zao kwani wajasiriamali wengi wanakosa ubunifu na kuiga kunakopelekea kuzalisha bidhaa za aina moja bila kufanya utafiti wa masoko.

Kupanda kwa bei na kutokuwepo viwanda vya vifungashio inakua ni kikwazo kikubwa kwa wajasiriamali na kupelekea bidhaa zao kuwa na bei ya juu ambapo wanakosa soko kulinganisha bidhaa kama hizo zinazotoka nje ya nchi. Kutokuwepo kwa udhibiti wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi kunapelekea bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara wa ndani kukosa soko. Baadhi ya Mifumo ya kisera na kisheria iliyopo inanyima fursa ya udhibiti wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi ambayo inapelekea bidhaa za wajasiriamali wa ndani kukosa soko. Vile vile, ufahamu mdogo wa soko na uhitaji kabla ya kutengeneza bidhaa ni changamoto nyengine inayowakabili wajasiriamali na wafanyabiashara nchini. Pia, wajasiriamali wanakosa taarifa sahihi za masoko ya bidhaa zao.

### 2.3.1. Udhibiti Ubora

Udhibiti ubora ni tendo la kuhakikisha kwamba bidhaa na huduma za kampuni fulani zinajengwa na kutolewa kwa Wateja/walaji kwa viwango stahiki, kwa muda muafaka kwa gharama inayokidhi (nafuu). Mawazo ya kuboresha udhibiti wa viwango unajumuisha, mchakato mzima wa kuandaa nyaraka, kufunza na kusimamia Vijana (Watumishi) wakati wa kuajiri, kuongeza ngazi za mafunzo kwa watumishi pale yanapohitajika, kuangalia bidhaa/huduma uwiano wake mara kwa mara, kuhakikisha kwamba vifaa (Mnyororo wa thamani) vinapatikana kwa wakati wote, kuanzisha ratiba na kuzisimamia. Manufaa ya kudhibiti ubora yanajumuisha ongezeko la unyenyekevu na mazungumzo ya wateja kuridhishwa na biashara nzuri, faida inayotokana na biashara, kulinda na kuboresha nafasi ya soko, kuboresha usalama wa mazingira ya kazi, kupunguza athari za madeni, kuchangia na kuwa na jina zuri la biashara (bidhaa/huduma).

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeunda Taasisi ya Viwango ya Zanzibar na Wakala wa Dawa, Chakula na Vipodozi ya Zanzibar ili kusaidia wajasiriamali katika uelewa mpana na uthibitisho ili waweze kutimiza wajibu wao wa kijasiriamali. Kuna haja ya ZBS na ZFDA na Shirika la Viwango la Tanzania na Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Tanzania kuendeleza mashirikiano ili waweze kuwa na mahusiano na ushirikiano mzuri. Uhusiano huo utatoa viwango sawa ambavyo vitahamasisha na kuelewa kwamba kila shirika baada ya kuthibitishiwa bidhaa au huduma yake litatambua uthibitisho wa viwango vya ubora kwa upande mwingine, hii itasaidia muendelezo wa kuwezesha Vijana wetu wajasiriamali wa Zanzibar. Changamoto iliopo ni kwamba Taasisi zinazosimamia wajasiriamali hazishirikiani ipasavyo na Taasisi za viwango nchini. Pia, kuna tatizo la kuwekwa kiwango kikubwa cha gharama ya kuthibitisha ubora wa bidhaa zao na upatikanaji wa alama za ubora.

Muundo huo unalenga kwenye kuboresha ubora wa bidhaa ikiwepo vifungashio pamoja na kuangalia uwiano wa ujazo wa bidhaa kwa mujibu wa usambazaji na matakwa ya bidhaa. Wajasiriamali wanahitaji kufuata na kujihusisha zaidi na Shirika la Ubora wa viwango la Zanzibar kuthibitisha na kuboresha ubora wa bidhaa zao kwa ajili ya soko zuri. Changamoto iliopo ni kwamba kuna uhaba wa upatikanaji wa vifungashio nchini na kupelekea wajasiriamali kuagiza Tanzania Bara ama Kenya kunakopelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa zinazozalishwa nchini na kuzorotesha soko.

### 2.3.2. Mnyororo wa Thamani

Katika kuhakikisha upatikanaji wa soko kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar, kuna umuhimu wa kuzingatia uwezeshwaji wananchi kiuchumi kwa mfumo wa kuzingatia mnyororo wa thamani. Zanzibar ina bidhaa muhimu kama viungo, chumvi, samaki, mwani na matunda kwa uchache zitakuwa na manufaa makubwa na kuweza kuongeza ukuaji wa uchumi wa Nchi na maendeleo ya raia wetu endapo yatachakatwa na kuongezewa thamani. Ukuaji wa biashara ya usafirishaji wa viungo nje ya Nchi, itahitaji teknolojia na ubunifu juu ya ukaushaji wa viungo hivyo, kuvichakata na kufungasha. Inatarajiwa ukuaji katika soko la viungo (spice) litakuwa na uhusiano mkubwa sana na Utalii, hoteli, viwanda vya uchakataji na ufungashaji kwa Zanzibar na kuzalisha ajira na itasaidia sana katika kuondoa umasikini.

Kuna sababu nyingi ambazo zinaelezea mahitaji ya kuongeza thamani na soko la bidhaa. Ili kutimiza ongezeko la mahitaji ya kuongeza thamani kwa bidhaa, wazalishaji na wasafirishaji wanatakiwa kujikita katika mahitaji ya wateja wetu kulingana na vipato vyao, ladha zao, mahitaji mahususi na vikwazo vya kiutamaduni na dini au vyote kwa pamoja.

Kwa sasa, mazao ya uvuvi na kilimo yanauzwa bila kuchakatwa na hata yale yanayochakatwa ni kwa kiwango cha chini sana. Mazao kama mwani, lulu na vito vinavyotokana na chaza ni miongoni mwa mazao yanayochakatwa kwa kiwango kidogo ama cha chini sana. Kwa kuongezea, samaki na mazao mengine yanachakatwa kwa kutumia njia za kienyeji za kuanika juani, kwenye mvuke na kutumia chumvi (Zanzibar Research Agenda 2015-2020). Kwa bahati mbaya viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu vina uwezo mdogo na teknolojia hafifu.

Sekta ya mboga mboga na matunda ya Zanzibar inaundwa na idadi kubwa ya wazalishaji wadogo wadogo ambao wanazalisha kiasi kidogo cha mboga mboga na matunda. Katika nchi nyingi zinazoendelea, Matunda yaliyoandaliwa vizuri na viwanda vya mboga mboga inakuwa kipengele muhimu sana katika biashara ya mazao ya chakula. Zanzibar inahitaji viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo katika eneo hili. Shughuli za viwanda kwa Zanzibar imejikita sana katika uchakataji wa biashara ndogo na za kati kwa bidhaa za ndani ikiwemo Usindikaji wa chakula,vinywaji na mchakato mzima wa mazao ya kilimo.

Kwa mujibu wa Zanzibar Research Agenda (2015-2020), uzalishaji wa maziwa kwa Zanzibar unakadiriwa kufikia tani 36,544 kwa mwaka, ambapo kati ya hizo hakuna zilizosindikwa.

Tena kiasi cha ng'ombe 14,800, mbuzi 3,000 na kuku Milioni Moja wanachinjwa Zanzibar kila mwaka bila kufuata taratibu za kuchakata. Kuongeza thamani kwa mazao tofauti ni muhimu ili kuepuka upotevu wa vifaa katika mchakato wote wa uzalishaji na uboreshaji wa ubora wa bidhaa.

#### 2.3.3. Makongano ya Kiuchumi

Njia ya kujigawa katika Makongano inatumika sana kuhamasisha MSMEs na kuchochea ukuaji wa kiuchumi kwa kuongeza manufaa ya viwanda yatakayopatikana katika Sekta na ukanda fulani. Kwa Zanzibar njia hiyo haijachukuliwa na kutumiwa ipasavyo katika sehemu za uzalishaji. Kundi ambalo linawakilisha sehemu katika uchumi litakuwa na sauti kwa Serikali kuliko mtu mmoja mmoja au hata vyama vingekuwa na vikundi vya kwao. Makongano yanahusisha shughuli nyingi, kama uzalishaji na maendeleo yake ya usambazaji bidhaa, utafiti wa kitaalamu wa masoko, huduma za kulea na kukuza biashara, mafunzo ya biashara na usimamizi wake, utafiti wa pamoja na maendeleo ya miradi na masoko.

Makongano haya yameanzishwa Zanzibar tangu 2006, ambapo Kongano la kwanza lilikuwa ni la wakulima wa Mwani. Kwa sasa, kuna makongano manane yanayojumuisha utengenezaji wa sabuni, asali, dagaa, matunda na mboga mboga, utalii, viungo, ufugaji wa kuku na mwani. Makongano haya bado ni machanga na yanakosa uwezo wa muundo wa kiusimamizi pamoja na uzalishaji mdogo. Kiujumla, dhana ya makongano na mipango yake ni dhaifu na kuna haja ya kuleta utaalamu ili kuwasilisha dhana hiyo.

#### 2.3.4. Ununuzi

Eneo la masuala ya manunuzi pamoja na taratibu za manunuzi za Serikali lina mchango mkubwa katika kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo na viwanda vidogo kuongeza maendeleo ya uchumi wa Wananchi wazawa. Aina hii ya juhudi za makusudi inahitaji 'database' ya bidhaa za Zanzibar, makampuni madogo na ya kati yanayomiliki biashara ili mfumo uweze kuongeza nguvu katika ukuaji. Taratibu za kimanunuzi sharti zizingatiwe kwa mujibu wa Mpango wa manunuzi na viwango vya bidhaa. Manunuzi hasa katika Taasisi za Umma yamekuwa na urasimu na yenye ushindani mgumu kiasi kwamba zabuni nyingi za Serikali zinashikiliwa na makampuni ya kigeni. Hali hii haina tija kwa sababu malipo yanafanywa kwa makampuni husika na kusafirishwa moja kwa moja kwenye Nchi zao kuongeza mapato ya Mataifa yao. Serikali na wakala wengine wa maendeleo wanatakiwa kusaidia bidhaa za ndani zinazomilikiwa na MSMEs.

### 2.4 Fedha na Mitaji ya Uwezeshaji.

Idadi kubwa ya Wajasiriamali ni masikini bado wana mbinu duni za upatikanaji wa huduma za kifedha zikiwemo Uwekaji akiba, Mkopo au hisa kutoka Taasisi ndogo ndogo za fedha hasa kutoka maeneo ya Vijijini.

Wanaume wana fursa nyingi kuwa na Ajira binafsi kuliko Wanawake kutokana na vikwazo vingi vikiwemo mtaji mdogo kwa ajili ya kuanzisha biashara na fursa chache za kupata mikopo kutoka Taasisi za fedha kama vile Benki, Vyama vya Ushirika vya kuweka akiba na kukopa (SACCOS) na vyanzo vingine. Ripoti ya FinScope ya mwaka 2017 inaonesha kuwa asilimia 38 ya Wazanzibari wanatumia simu za mkononi kufanya huduma za kifedha wakati asilimia 15 hutumia Benki. Imegundulika kuwa asilimia 2 wanatumia Taasisi ndogo za kifedha na asilimia 1 pekee wanatumia SACCOS kwa huduma za kifedha. Inaonesha zaidi kuwa asilimia 53 wanaume na asilimia 36 Wanawake ndio wanaotumia huduma hizo za kifedha.

Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogo, wadogo wadogo na wakati (SMEs) wanahitaji kusaidiwa kifedha kwa kuzipatia mitaji ya kuanzisha na kuimarisha biashara zao. Utoaji wa mikopo wenye masharti nafuu ni muhimu sana kwa sababu ni wachache tu ndio wanaweza kuwa na dhamana za kuweka kwenye benki ili waweze kupata mikopo yenye viwango vya juu vya riba. Ukamilishaji wa Sera za fedha ndogo ndogo itaimarisha ushirikishwaji wa kifedha ikiwemo miongozo ya utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa wajasiriamali.

Kuna aina mbali mbali za mitaji, lakini katika sera hii, mtaji unatambuliwa kuwa ni fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za kiuchumi. Wajasiriamali wengi hivi sasa ukiwauliza nini changamoto zao katika shughuli wanazozifanya watakwambia ukosefu wa mtaji. Hii inaweza kuwa ni changamoto lakini changamoto hii ina sababu ambazo ndizo zinawafanya wajasiriamali kusema wanakabiliwa na ukosefu wa mitaji.

Wajasiriamali wengi wanapata changamoto kubwa katika kupata mitaji ya kuanzishia biashara. Ni vigumu kuanzisha biashara bila kuwa na mtaji wa kutosha, hivyo basi mtaji ni muhimu sana ingawa mtaji pekee hautoshi kuanzisha biashara ni lazima uwe na elimu ya ujasiriamali ili uweze kufanikiwa katika biashara. Kuna njia mbali mbali za kupata mtaji ambazo mjasiriamali anaweza kuwa na mtaji wake mwenyewe kabla hajaanza biashara au faida inayotokana na biashara inayoendelea. Anaweza pia kupata mtaji kwa hisa alizowekeza katika kampuni lakini hii sio njia maarufu hasa kwa wajasiriamali wadogo. Njia nyingine ya kupata mtaji ni kupitia mikopo kutoka benki au Taasisi nyengine za kifedha zikiwemo SACCOS. Hizi ni njia maarufu sana hapa Zanzibar. Wananchi wengi wamekuwa wakipatiwa huduma za mikopo kupitia Taasisi za Serikali za Uwezeshaji kutokana na uwepo wa masharti nafuu ya huduma hiyo.

Mikopo yote hii imekuwa na changamoto mbali mbali ambazo zimesababisha lengo la kuwawezesha wanachi kiuchumi kutofikiwa kama ilivyokusudiwa. Mikopo ya Benki inatolewa pamoja na riba kubwa sana ambayo ni mzigo kwa wajasiriamali kurejesha kwa wakati. Pia, upatikanaji wake unahitaji kuweka dhamana ambazo wajasiriamali wengi wanashindwa kukopa Benki kwa kukosa dhamana. Kutokana na masharti hayo magumu wajasiriamali wengi hawapendi kupata mikopo kupitia mabenki, kwa sasa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umeelemewa kutokana na mahitaji mengi ya mikopo wakati uwezo uliopo ni mdogo na hauwezi kuhudumia maombi yote. Kwa wastani kiasi cha asilimia

15 tu ya maombi ndio yanayoweza kuhudumiwa hii inaonesha ukubwa wa tatizo la ukosefu wa mitaji liliopo.

Tathmini za wakopaji na wajasiriamali katika Taasisi mbali mbali za fedha inaonesha kuwa wananchi wengi wa Zanzibar hawapendi kukopa benki kutokana na riba. Ndio maana wanakimbilia kwa wingi katika Taasisi za uwezeshaji ambapo gharama za mikopo zinapungua.

### 2.5 Ajira na Fursa za Ajira

Zanzibar kama nchi nyengine Duniani inakabiliwa na tatizo la upungufu wa Ajira kwa Wananchi wake hasa Vijana. Ajira nchini zinazalishwa kupitia Sekta Rasmi, Sekta Binafsi na Sekta isiyo Rasmi. Nguvu Kazi iliopo nchini imeshuka kutoka asilimia 79 mwaka 2014/2015 hadi asilimia 76 mwaka 2021. (Matokeo ya Awali ya Utafiti wa Nguvu Kazi 2021). Kwa mujibu wa Taarifa za Mtakwimu Mkuu wa Serikali (Zanzibar Statistical Abstract 2020), Waajiriwa wote wa Sekta Rasmi (Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi) kwa mwaka 2019/2020 ni 67,095 ambapo ni sawa na asilimia 10.8 tu ya ajira zote nchini hivyo, kuifanya Sekta isiyo rasmi kubeba mzigo mkubwa wa kuzalisha ajira hasa kwa Vijana. Vijana wengi nchini wanategemea ajira katika Sekta isiyo Rasmi (Ujasiriamali) ambapo Sekta isiyo Rasmi inaajiri asilimia 41.7 ya nguvu kazi nchini ambayo wengi ni Vijana. Hivyo, Serikali inatakiwa kuweka mikakati imara, madhubuti na endelevu ya kulishughulikia eneo hili.

Kwa mujibu wa takwimu za Awali za Utafiti wa Nguvu Kazi wa mwaka 2021, tatizo la ukosefu wa ajira limeongezeka kufikia asilimia 19.7 kutoka asilimia 14.4 ya mwaka 2014. Aidha, Utafiti huo umebainisha kwamba tatizo la ajira kwa Vijana limepanda kufikia asilimia 27.4 kwa mwaka 2021 kutoka asilimia 21.3 mwaka 2014. Takwimu hizi zinabainisha ukubwa wa tatizo la ukosefu wa ajira kwa Vijana nchini mbali ya jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Serikali za kutatua tatizo hilo.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kupambana na tatizo hili kwa kuweka lengo maalum katika utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara 136 (c) la kuzalisha ajira 300,000 ifikapo mwaka 2025. Lengo hili litaweza kufikiwa kwa kufanya mapitio ya Sera, Programu na Mipango mbali mbali za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itakayosimamia uzalishaji wa ajira zitakazowanufaisha wazawa hasa Vijana. Mipango na mikakati hiyo ni pamoja na kuweka vipaumbele maalum vitakavyoendelezwa kusimamia ukuwaji wa uchumi wa nchi, kuimarisha uwekezaji, kuimarisha upatikanaji wa fursa za ajira kupitia Uchumi wa Buluu na sekta nyengine zilizosahauliwa ambazo zinaweza kuzalisha ajira kwa Vijana kama michezo na utamaduni.

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inahitaji kuweka vipaumbele maalum vya uwezeshaji ambavyo vitaondosha tatizo la ukosefu wa ajira nchini na kuimarisha sekta ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Sekta hizo ni pamoja na:-

### 2.5.1 Elimu

Elimu ni Ufunguo wa Maisha ambapo ni muhimu kwa kufikia malengo ya kupambana na wimbi la tatizo la uhaba wa upatikanaji wa fursa za Ajira nchini. Takwimu zinaonesha kwamba, Mfumo wa Elimu uliopo unamfanya mwanafunzi kuwa mtegemezi wa ajira kutoka Serikalini au katika Sekta Rasmi ikiwemo Sekta Binafsi. Taarifa za Zanzibar Statistical Abstract 2020 zinaonesha kwamba jumla ya wanafunzi 23,165 walifanya Mtihani wa Kidato cha Nne lakini asilimia 13 tu ya wanafunzi hao wamefaulu kwa kiwango cha daraja la I-III na kufanikiwa kuendelea na Kidato cha Tano, hivyo kufanya asilimia 87 ya Vijana kubaki nje kutafuta njia nyengine za kujiendeleza ama kutafuta ajira. Takwimu hizi zinaonesha haja ya Serikali kuimarisha mifumo ya Uwezeshaji nchini ili kuokoa wimbi la Vijana linalokosa kuendelea na masomo nchini. Vijana hawa wakiachiwa wanaweza kujiingiza katika vitendo hatarishi ikiwemo matumizi ya dawa za kulevya. Aidha, ni muhimu kufanya mapitio ya Sera ya Elimu ikiwemo mitaala ili iingizwe dhana nzima ya Ujasiriamali, kuimarisha vyuo vya amali na vyuo vya ufundi na kusimamia vyema mafunzo kazi kwa Vijana, kuimarisha mitaala ya masomo ya sayansi, utafiti na ubunifu katika maskuli na vyuo vya elimu ya juu.

Kwa mujibu wa hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali 2020/2021, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendesha vituo vinne (4) vya Mafunzo ya Amali na Vituo 69 vya Mradi wa Sayansi kwa Unguja na Pemba ambavyo vinatoa ujuzi kwenye Mradi wa Sayansi na Ufundi Seremala.

Mafunzo hayo yamejikita katika fani mbali mbali kama vile Ufundi Seremala, uhunzi, upishi, ushonaji, uunganishaji umeme, Electronic, Automotive, Mechanics, domestic Electrical, Industry Electrical, Uvuvi, Ufugaji wa kuku na ngombe wa maziwa, huduma za mahotel na vinywaji, IT na ujenzi/ufundi uwashi. Kwa sasa maeneo mapya kama ujuzi wa matumizi ya kompyuta, uhasibu na utunzaji fedha yameanzishwa.

Kituo cha Kulea na kukuza Wajasiriamali huko Mbweni kinatoa mafunzo kwa wajasiriamali kwa kufundisha kozi kama programu za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya habari (TEHAMA), usindikaji wa mazao ya kilimo, uokaji na ujasiriamali. Ni muda muafaka sasa kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) kuingiza Programu ya Ujasiriamali katika mitaala yao na kuanzisha somo la Ujasiriamali kuanzia ngazi ya elimu ya msingi. Elimu Mbadala na Elimu ya Watu wazima ina vituo 2, kituo cha Elimu mbadala Rahaleo na cha elimu ya watu wazima kilichopo Forodhani.

### 2.5.2 Uchumi wa Buluu

Dhana ya Uchumi wa Buluu ni pana ambayo imebeba shughuli zote za msingi zinazofanywa katika bahari kama vile, uvuvi wa aina mbalimbali ukiwemo wa kibiashara na usio wa kibiashara katika kina kirefu na kifupi cha maji, Shughuli za usafirishaji Baharini, uvunaji wa chumvi, Shughuli za Mwani, Ufugaji wa Samaki kwa kupitia Mabwawa, Shughuli za utafutaji na uchimbaji wa Madini na Mafuta Baharini. Pia, shughuli zote za starehe na michezo kando kando mwa bahari, Shughuli za bandari na upana wake pamoja na Masuala

mengine kama vile ujenzi wa vyombo vya baharini kama Meli na Boti, Viwanda, elimu na tafiti kuhusu bahari.

Uchumi wa Buluu unafaida kubwa katika ukuzaji wa Uchumi wa nchi ambapo huongeza pato la taifa na pato la mwananchi mmoja mmoja. Serikali imeweka mikakati mbali mbali ya kuimarisha Sekta hii ikiwemo kuweka vivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje wanaotaka kuwekeza katika Sekta hii. Hivyo, ni vyema kuweka mikakati maalum ya kuwawezesha Wazawa kuweza kusimamia na kuingia katika Sekta hizi ikiwemo mafunzo, kuwapa mitaji na kuwataafutia masoko ya bidhaa watakazozalisha. Serikali imeweka kipaumbele cha kuwawezesha wananchi katika baadhi ya mazao yenye tija kwa kukuza uchumi wa nchi ikiwemo uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha mwani, ufugaji wa samaki na majongoo, uvunaji wa chumvi, viwanda vidogo vidogo vya kusindika bidhaa hizo na kukuza ubora wa bidhaa na masoko kama mwani, chumvi, majongoo ya bahari na dagaa. Suala la kuongeza thamani ya mazao hayo ni la muhimu sana kwani eneo hili likisimamiwa ipasavyo linaweza kuzalisha ajira kwa wingi. Wazawa wapewe fursa ya kuingia ubia na wawekezaji wenye uwezo wa kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu na viwanda vya kusindika mazao ya bahari.

Mafuta na Gesi ni moja ya Sekta zilizo chini ya dhana ya Uchumi wa Buluu ambayo inaweza kuzalisha fursa mbali mbali za Ajira kwa Vijana. Serikali imeweka mikakati madhubuti na imara kwa Vijana kuweza kuzitambua na kuzitumia fursa zitakazojitokeza katika Sekta hii wajifunze stadi mbalimbali ili waweze kupata ajira hususan katika sekta isiyo rasmi. Kufuatia tafiti za awali za ugunduzi wa mafuta kumekuwa na mahitaji ya waajiriwa katika sekta hiyo. Hivyo ni vyema Vijana kuwa na stadi zinazohitajika ili kuweza kupata ajira katika sekta hiyo changa ya mafuta na gesi. Aidha, kuna changamoto ya kuweza kufanya tathmini ya mapema ni maeneo ya gani ya uwezeshaji wa jamii kusimamia uendelezaji wa Sekta hii ambayo wananchi wanahitaji kutayarishwa kuzitumia fursa za uwezeshaji katika maeneo hayo. Serikali iweke utaratibu wa kuwajengea uwezo wananchi kuweza kuwekeza katika Sekta ya Mafuta na Gesi ili kuweza kuwaandaa na kuwawezesha wazawa kuzichangamkia fursa za ajira.

Serikali isimamie uwezeshaji wa wananchi kwa kuwajengea uwezo na kuwakusanya pamoja kupitia makongano mbali mbali kwa mujibu wa Sekta za kipaumbele kutakakorahisisha upatikanaji wa mafunzo, mitaji na masoko kwa wanavikundi na wajasiriamali.

### 2.5.3 Uwekezaji

Masuala ya Uwezeshaji nchini yanakwenda sambamba na Uimarishaji wa Uwekezaji katika nchi. Uwekezaji ukiwa mkubwa unaweza kuzalisha ajira nyingi sana nchini. Tokea kuanzishwa kwa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar hadi Agosti 2021, jumla ya miradi 1,110 imeanzishwa ambapo miradi hai ni 799 yenye Mtaji wa Makisio wa Dola Bilioni 7.5 inayokadiriwa kuzalisha ajira 59,259 kwa wazalendo. Sekta ya Utalii ina miradi 434 (54.3%) ya miradi yote. Hivyo, Serikali ifanye uwezeshaji kwa Wananchi kuzalisha bidhaa zilizo bora zitakazoweza kusambazwa katika Mahoteli yanayofunguliwa na maeneo mengine ya

uwekezaji. Kuimarisha uzalishaji kwa ujumla kuwa wa kisasa pamoja na kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Serikali iendelee kuimarisha Sekta ya Uwekezaji katika maeneo ya Sera, Sheria, Vivutio, Miundombinu, Wataalamu na Miongozo imara ya kusimamia ufanisi wa Sekta hii kwani ina maeneo ya uwezeshaji na ajira kwa Wananchi. Pia, kuna changamoto ya kutowaanda na kuwawezesha wananchi kuweza kushiriki katika miradi ya uwekezaji katika maeneo yao pamoja na kuingia ubia na wawekezaji.

### 2.5.4 Utalii

Ni Sekta ya kipaumbele inayosimamia ukuaji wa uchumi wa nchi na ukuaji wa pato la mwananchi. Kwa mujibu wa takwimu zilizopo za mwaka 2020, Utalii umechangia asilimia 43.9 kupitia Sekta ya Huduma ikifuatiwa na kilimo asilimia 27.6 na Sekta ya Viwanda asilimia 19.3. Utalii unatoa na kuzalisha fursa nyingi sana za ajira kupitia Uwekezaji na Uwezeshaji nchini ikiwemo Hoteli, Michezo ya Ufukweni, Mikahawa, Kutembeza Watalii, Sanaa, Utamaduni, Mawasiliano, Usafirishaji na Mabenki. Miundombinu ya Utalii na suala la ukarimu vinaweza kuzalisha fursa za ajira kwa Vijana. Vijana walioajiriwa wenye Umri wa miaka 15-35 katika kutoa huduma za Malazi na Chakula ni asilimia 10.2 na wengi wao ni Wanawake asilimia 15.7 (ILFS 2014/2015).

Utalii wa baharini unajumuisha michezo ya bahari na ufukweni, kuogelea, kurusha vishada, kusafiri kwa kutumia boti na kutembeza wageni. Uwekezaji katika upande wa michezo ya bahari na ufukweni bado haujapewa kipaumbele cha kutosha wala matumizi ya Sanaa na Utamaduni ambavyo ni vivutio vikubwa kwa Watalii. Ni vyema Serikali ikawezesha jamii hasa Vijana kuwekeza katika eneo hili kwa kuwapatia Mitaji au kuingia Ubia na Wawekezaji. Kwa mujibu wa takwimu, Sekta ya Utalii inaweza kuzalisha ajira 35,000 kwa mwaka 2019 (Dira 2050). Suala la Mafunzo Kazi kwa Vijana katika Sekta ya Utalii lipewe kipaumbele cha pekee ili kuwaimarisha na kuwawezesha Vijana kuingia katika Sekta hii kuendana na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira.

Pia, Sekta ya Utalii inaweza kutoa ajira zisizo za moja kwa moja katika shughuli kama za usambazaji wa vyakula kwenye mahoteli, migahawa, makampuni ya ujenzi ambayo yanajenga na kukarabati maeneo ya watalii na miundombinu, wachongaji, kazi za mikono, madalali wa masoko na huduma za fedha. Pia, kuna fursa ya kuboresha utalii wa kiuchumi ambapo Wazanzibari wengi watawezeshwa ili waweze kuingia katika biashara. Sekta ya Michezo na Utamaduni ni sehemu muhimu katika kuzalisha ajira nchini. Sekta hizi bado hazijasimamiwa ipasavyo kama ni sehemu ya uwezeshaji kwa Vijana nchini.

### 2.5.5 Kilimo

Kilimo kinaendelea kuchukua nafasi ya pili katika kuchangia Pato la Taifa kwa asilimia 22.8 kwa mwaka 2020. Kilimo katika Sera hii kinakusanya ukulima wa mazao (mazao ya chakula, matunda, viungo na mboga mboga) na ufugaji wa wanyama kwa ajili ya chakula na biashara pamoja na misitu. Kwa mwaka 2020 jumla ya ekari 100,907 zilitumika kwa kilimo cha mazao ya chakula, matunda na mboga mboga ambazo zilizalisha tani 396,014.02. Pia, sekta

ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 iliweka msingi wa uhakika wa usalama wa chakula kwa asilimia 48.9. Serikali inaendelea kuwekeza na kuimarisha Sekta ya kilimo ili iweze kuwavutia watu wengi hasa Vijana kwa kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo, mashine, kujenga uwezo, kuweka miundo mbinu ya kisasa ya kilimo na umwagiliaji, kujenga uwezo wa kuzalisha mazao bora na wanyama pamoja na kuimarisha masuala ya utafiti na mafunzo.

Mbali ya jitihada zote hizo lakini bado Sekta hii inakabiliwa na changamoto mbali mbali ikiwemo mwenendo unaosuasua wa uzalishaji, uzalishaji mdogo na ubora wa mazao ambao haukidhi soko, na uhaba wa ardhi ya kutosha kwa kufanya kilimo cha biashara kinachoendana na soko. Vijana wengi wanaikimbia Sekta hii kutokana na kuwa haina tija na inachukua muda mrefu kuona tija.

Kilimo ni chanzo muhimu cha Ajira katika Visiwa hivi. Kwa Wastani, asilimia 70 ya watu wa Zanzibar wanategemea sekta ya kilimo moja kwa moja au sio moja kwa moja kwa maisha yao. Kiasi cha asilimia 37.5 ya Vijana kati ya umri wa miaka 15-35 wameajiriwa katika kilimo, misitu na uvuvi. Hivyo, Vijana hawa wanatakiwa kuwekwa katika makongano kwa mujibu wa mazao wanayozalisha na kujengewa uwezo wa kuzalisha bidhaa zinazoendana na kwa kiwango kinachohitajika na soko Zanzibar, Afrika mashariki na hadi Kimataifa. Programu za Uwezeshaji zinaweza kuandaliwa kwenye uzalishaji na usafirishaji, upelekaji wa bidhaa za kilimo Nje ya Nchi, Ajira katika biashara ya kilimo, kuongeza Thamani kwenye mazao ya kilimo na program za msaada wa Kifedha katika kilimo, vikiwemo vyama vya ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na nyenzo kwa mikopo midogo midogo. Serikali ni vyema kuweka mikakati maalum ya kuwawezesha Vijana wanaojishughulisha katika Sekta kupata mitaji itakayoweza kuwasaidia kuimarisha uzalishaji.

Sekta nyengine ambayo ni muhimu kwa uwezeshaji wananchi kiuchumi ni misitu ambapo zao la asali ni zao lenye tija kubwa sana katika soko la ndani na la nje. Changamoto iliyopo ni uzalishaji hafifu usioendana na mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi. Sekta ya misitu inahitaji kuwekewa kipaumbele sawa na sekta nyengine za kilimo ili kuweza kuleta tija. Na ili kufikia lengo hilo, Serikali iweke mikakati ya kuanzisha na kuliimarisha Kongano la Wazalishaji Asali nchini.

### 2.5.6 Viwanda.

Shughuli za viwanda Zanzibar zimejikita katika viwanda vidogo vidogo na vya kati na viwanda vilivyopo ni pamoja na viwanda vya usindikaji chakula, vinywaji na mazao ya kilimo. Pia, sekta hii inajikita na uchimbaji wa mchanga na kokoto, utengenezaji wa bidhaa, kuzalisha umeme, gesi na maji. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Zanzibar ina jumla ya viwanda 2,201 ambapo vimeajiri Wananchi 10,427. Kati ya idadi ya viwanda hivyo 5 ni viwanda vikubwa (Sensa ya Viwanda 2014 – OCGS). Taarifa za Zanzibar Statistical Abstract ya mwaka 2020 imebainisha kwamba uzalishaji wa viwandani umeongezeka kama ifuatavyo: Vinywaji asilimia 1.2; Mikate asilimia 2.0; Unga wa ngano asilimia 17.5; Bidhaa za maziwa asilimia 2.1; Tambi asilimia 6.63 na mafuta ya mimea asilimia 2.0. Ongezeko hili limetokana na mahitaji ya soko la ndani.

Viwanda ni eneo muhimu linaloweza kukuza uwekezaji na sekta ya uwezeshaji nchini. Wazawa wawezeshwe kwa kujengewa uwezo na kupewa mitaji ya kuanzisha viwanda vidogo na vya kati kwa mujibu wa sekta za uchumi zilizopewa kipaumbele na Serikali. Viwanda vya kupewa kipaumbele zaidi ni vile rasilimali zake zinaweza kupatikana nchini kama vile mwani, matunda, mazao ya baharini, viungo, chumvi na karafuu. Serikali iendeleze taratibu za kutenga maeneo/ardhi maalum ya viwanda ikiwa ni mkakati wa uwezeshaji ili kuweza kutoa fursa kwa wawekezaji wa ndani na wa nje. Aidha, kuwepo na uhamasishaji na uwezeshaji kwa wananchi kuweza kuzalisha bidhaa za malighafi zinazohitajika viwandani pamoja na kusimamia masoko ya bidhaa zitakazozalishwa. Vijana wajengewe uwezo wa kuzichangamkia fursa zilizopo ikiwemo kusimamia usafirishaji wa bidhaa zitakazozalishwa nje ya nchi. Changamoto iliopo hakufanywi tathmini ya kina kwa mahitaji ya masoko ya bidhaa za viwanda tunazozalisha kabla ya kuvianzisha.

### 2.6 Ubunifu na Kuasili Teknolojia ya Kisasa

Ubunifu wa wajasiriamali unategemea kuongezeka kwa teknolojia na uvumbuzi. Wataalamu wengi wa biashara wanakubali kwamba ubunifu ni muhimu kwa mafanikio ya mawazo haya kwa kiwango kikubwa na kubadili dhana. Dunia ya sasa imetawaliwa na mawazo ya kiubunifu na teknolojia mpya, lakini ubunifu pekee hauwezi kufanikisha mafanikio. Wabunifu wanahitaji msaada mkubwa kufanya mawazo yao na kutafuta fursa mpya na zenye tija. Vile vile, uanzishaji wake unahitaji fedha ili waweze kuanza biashara zao mpaka muda wa kuanza kujitengenezea mapato yake yenyewe.

Wawekezaji wanaangalia miradi yenye nguvu ya kijasiriamali na kuwekeza pekee katika bidhaa/mazao maalum/muhimu. Wazo zuri na lenye uwezo wa kushawishi linaweza kusaidia kuanzisha wawekezaji wenye faida ambao unaweza kuwasaidia kupanua malengo ya biashara zao. Changamoto iliopo ni kutokuwepo kwa miundombinu ya kuendeleza vipaji vya ubunifu wala mitaji/fedha za kusaidia uzalishaji.

Utafiti na ubunifu ni vitu muhimu katika kuboresha ubora wa mazao. Kwa sasa, Serikali imefanya juhudi mbali mbali kutambua na kuendeleza wajasiriamali wenye vipaji ikiwemo usaidizi wa vifaa, ujuzi na matumizi ya teknolojia ya kisasa. Taasisi kama Tume ya Sayansi (COSTECH), Taasisi za Elimu ya juu na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatakiwa kufanya kazi kubwa kuchochea wajasiriamali kuwa wabunifu zaidi. Kwa hiyo, mtu anaweza kufikiria kwamba teknolojia inayoanzishwa itabaki na kuweza kusaidia katika kuchangia katika michakato ya mara kwa mara ya uvumbuzi na ya maendeleo ya teknolojia.

### 2.7 Muundo wa Kitaasisi na Uratibu

Mipango ya uratibu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi Zanzibar ipo chini ya Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Wakala-unaoshughulikia masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Hapa Zanzibar kuna Taasisi nyingi za umma na binafsi ambazo zinashughulikia masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuona wananchi hao

wanakuwa na mchango unaofaa katika kuimarisha kipato chao na uchumi wa nchi kwa jumla.Wakala u~~i~~na~~y~~osimamia shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unatakiwa kuratibu na kufuatilia shughuli za Uwezeshaji Kiuchumi nchini lakini uwezo wake ni mdogo. Kwa jumla, Serikali na Taasisi zisizo za Kiserikali zinazoshughulika na mambo hayo zimegawanyika ~~na~~ na hazifuatilii vizuri shughuli zinazofanywa na Wadau mbali mbali jambo ambalo linapelekea shughuli moja kufanywa na Taasisi zaidi ya moja. Hivyo, kuna haja ya kuimarisha mfumo wa Kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa programu na shughuli za Uwezeshaji Kiuchumi katika Taasisi zote za Umma na Binafsi kwa ngazi mbalimbali za kiutendaji. Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi ni muhimu kwa maendeleo ya wajasiriamali wadogo, wakati, wafanyabiashara wakubwa pamoja na kuondoa umasikini Zanzibar.

Aidha, kutokuwepo kwa mashirikiano ya kutosha ya kiutendaji baina ya Taasisi moja na nyengine jambo ambalo husababisha ugumu katika kufikia malengo ya Taasisi husika za utoaji huduma za kuwawezesha wananchi kiuchumi.

## 2.8 Mifumo ya Kisera na Kisheria

Ukuaji wa Uchumi endelevu wa Zanzibar unahitaji kwenda kwa pamoja na maendeleo ya Uchumi wa watu wake. Mifumo ya Kisera na Kisheria ni vyombo muhimu sana katika utekelezaji sahihi wa program za uwezeshaji kiuchumi. Kuna Sera nyingi za Nchi na za Sekta mbali mbali zinazoelezea umuhimu wa kuwawezesha wananchi wa Zanzibar. Kwa hiyo, ni muhimu kuratibu programu na shughuli za uwezeshaji ziwe katika mfumo mmoja utakaojitosheleza kwa kina.

Sera hii itahimiza watu kutumia kikamilifu fursa za kiuchumi sio tu kwa maendeleo yao lakini pia kwa maendeleo ya jamii yote kwa ujumla. Lengo ni kusaidia watu wazitambue fursa zao muhimu za kiuchumi kuleta ukuaji endelevu kwa Zanzibar na kuboresha maisha yao na hivyo, kuleta mfanano katika mgawanyo wa manufaa yatokanayo na uchumi wa Taifa. Maendeleo ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yatakwenda pamoja na utungwaji wa Sheria ya Uwezeshaji Kiuchumi ambayo itasimamia vizuri na kikamilifu utekelezaji wa sera hii.

## 2.9 Masuala Mtambuka

### 2.9.1 Jinsia

Usawa wa jinsia na uwezeshaji wa Wanawake ni mambo makuu ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayaangalia kwa jicho la karibu sana. Wanawake wanafanya karibu asilimia 51.6 ya idadi ya watu nchini lakini bado sehemu kubwa haifaidi kuzitumia fursa za kiuchumi zilizopo kutokana na maumbile pamoja na mila desturi zilizojengwa na jamii. Kati ya asilimia 27.4. ya Vijana wenye umri kati ya miaka 15-35 waliokua hawana ajira nchini, asilimia 40.6 ni Wanawake. Asilimia 23.7 ya Kaya Zanzibar zinaongozwa na Wanawake na asilimia 55.2 ya hao bado wapo katika ndoa ~~bado~~ (HBS 2019/2020). Wanawake wengi wanajishughulisha na ajira zisizo rasmi na Wanawake wa vijijini ndio zaidi (52%).

Changamoto iliyopo Programu za Uwezeshaji haziweki kipaumbele maalum kwa kundi hili. Hivyo, Watekelezaji wote wa Mipango na Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa ngazi zote na kwa Sekta za Umma na Binafsi ni muhimu kuzingatia masuala ya jinsia tangu hatua za awali za uandaaji wa programu pamoja na kuhakikisha kuwa kila mpango au programu unanufaisha wote (Wanawake na Wanaume) wakiwemo Watu wenye Ulemavu na kwa kuzingatia maeneo yaliyoathirika zaidi baina ya Mjini na Vijijini.

### 2.9.2 Vijana

Vijana ndio nguvu kazi ya Taifa na ndio waathirika wakubwa wa ukosefu wa ajira nchini. Zanzibar ina kiwango cha ukosefu wa ajira cha asilimia 19.7 na asilimia 27.4 ni kwa Vijana wenye umri wa kati ya miaka 15-35 kati ya hao asilimia 40.6 ni Wanawake (Matokeo ya Awali ILFS2021. Kwa mujibu wa takwimu za makadirio ya Idadi ya Watu nchini kwa mwaka 2020 Vijana Zanzibar wanafanya asilimia 35 ya watu wote. Pia, utafiti wa (HBS 2019/2020) umebainisha kwamba asilimia 45.4 ya kaya zinaongozwa na Vijana kuanzia miaka 15-35. Aidha, umebainisha kwamba asilimia 87 ya Vijana wanakuwa hawawezi kuendelea na masomo yao kutokana na kutokufaulu mitihani yao ya kidato cha nne. Hali hii inapelekea kuwepo na idadi kubwa ya Vijana mitaani wakizurura bila ya shughuli yoyote na kufanya mzigo mkubwa kwa Serikali kuwa na wimbi la Vijana waliokosa ajira. Hivyo, Sera itaweka mifumo na miongozo ya uwezeshaji wa Vijana kwa kuweka miundo mbinu ya mafunzo kiwilaya, kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na biashara, upatikanaji wa mitaji na masoko, kuimarisha ubunifu na matumizi ya TEHAMA ili kuweza kuanzisha na kusimamia miradi yao mbali mbali ya uwezeshaji kwa mujibu wa sekta za vipaumbele vya ukuzaji wa uchumi zilizowekwa na Serikali. Pia, itaratibu kwa pamoja upatikanaji wa mafunzo ya amali na mafunzo kazi kwa Vijana kwa mujibu wa mahitaji na soko la ajira nchini na nje ya nchi.

### 2.9.3 VVU/UKIMWI na Dawa za Kulevya

Takwimu za Tume ya UKIMWI 2020 zinaonesha kwamba Zanzibar ina kiwango cha chini cha maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) (0.7). Hata hivyo licha ya kuwepo kwa maambukizi madogo, lakini nguvu kubwa hivi sasa inaelekezwa kwa makundi maalumu ambayo kiwango cha maambukizi ni makubwa. Makundi hayo ni akina mama wanaofanya biashara ya ukahaba asilimia 19.3, akina baba wanaofanya mapenzi ya jinsia moja asilimia 2.6 na Vijana wanaotumia dawa za kulevya kwa njia za kujidunga sindano kwa asilimia 11.7. Changamoto za kiafya na kijamii zilizotajwa zinaongezea hali ya Vijana kushindwa kumudu maisha yao na kuongeza hali ya umasikini zaidi. Kundi hili linahitaji kuwekewa mikakati maalum ya uwezeshaji ili kuweza kujikimu kimaisha na kuacha kusambaza maradhi nchini.

Serikali inaendelea na mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kuweka mikakati mbali mbali ya kuzuia na kuchukua hatua za kuwatoa Vijana waliojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Kwa mujibu wa taarifa ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali (Zanzibar Statistical Abstarct 2020) kuna jumla ya sober house 6 zenye watumiaji 349 ambao wote ni wanaume ambapo watumiaji hawa kati ya miaka 26 – 35 sera hii inatakiwa kuweka mikakati ya uwezeshaji ili kuwatoa Vijana hawa kufanya vitendo vya uhalifu.

### 2.9.4 Watu Wenye Ulemavu

Zanzibar ina watu wengi wenye ulemavu ambao wanafikia asilimia 5.8 (Sensa 2012). Wengi wao wanaishi katika kundi duni la kiuchumi na wanaishi chini ya mstari wa umasikini na hawawezi kumudu mahitaji ya msingi ya maisha. Ni wazi kwamba umasikini na ulemavu vina uhusiano wa karibu. Ulemavu wa aina mbali mbali unawakosesha kuingia katika fursa mbali mbali za kiuchumi au kuwa na fursa duni za kimaisha ambazo matokeo yake zinawafanya kuwa katika kundi la umasikini na utegemezi. Mara Nyingi watu wenye ulemavu (PWDs) wanaenguliwa au hawawezi kunufaika moja kwa moja na programu za kiuchumi na kijamii kutokana na kusahauliwa kuwekewa miundo mbinu itakayosaidia kunufaika na programu hizo. Taasisi zinazotoa huduma za masuala ya Uwezeshaji ziweke mazingira na miundombinu wezeshi kwa ajili ya kupata huduma mbali mbali zitakazosimamia ufanisi wa uzalishaji wa miradi yao ya uwezeshaji. Huduma za mafunzo, masoko na mitaji ziende sambamba na mahitaji yao. Sera iweke Mikakati ya kuwawezesha watu wenye ulemavu kiuchumi ili waweze kujikwamua kimaisha na kuondokana na utegemezi.

### 2.9.5 Mabadiliko ya Tabia nchi na Mazingira.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mikakati na inasimamia miongozo mbali mbali ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi na utunzaji wa mazingira nchini. Kutokana na shughuli mbali mbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi zitakazofanyika ni muhimu kuhakikisha tunafuata kanuni na sheria zote za utunzaji mazingira nchini. Harakati hizo zinaweza kupelekea mmongonyoko wa ardhi uchafuzi wa fukwe na bahari, uchache wa vyanzo vya maji, upotevu wa bioanuai, ukataji ovyo wa misitu na makaazi holela mijini. Hivyo, ni lazima programu za uwezeshaji ziende sambamba na kuongeza uelewa wa jamii wa kuhifadhi na kutunza mazingira nchini. Programu za kuotesha miti na usafi wa mazingira ziwe ni sehemu ya vipengele muhimu katika programu zote za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kwa ile miradi mikubwa suala la kufanya tathmini ya mazingira (Environmental Impact Assessment) litiliwe mkazo wa hali ya juu.

Masuala ya Uwezeshaji yatajikita katika sekta za viwanda, biashara, utalii, teknolojia ya habari na mawasiliano, kilimo, utalii, mafuta na gesi na uvuvi. Suala la kutunza uasili wa mazingira na tamaduni za nchi lipewe kipaumbele katika miradi ya Uwezeshaji Zanzibar. Miradi itakayowekezwa ifanyiwe tathmini ya kina ili kuelewa kwamba haitaleta athari ya mabadiliko ya tabianchi hapo baadae. Watendaji wajengewe uwezo wa kuweza kusimamia utekelezaji wa shughuli hizi na Taasisi inayosimamia masuala ya Uwezeshaji Wananchi ~~Wananchi~~ Kiuchumi ifanye kazi kwa karibu na kwa ufanisi na Taasisi zinazosimamia masuala ya mazingira na ardhi.

### 2.9.6 Ongezeko la Idadi ya Watu

Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni lazima zizingatie ongezeko la idadi ya watu sambamba na fursa mbali mbali za uwezeshaji zilizopo ikiwemo mafunzo, miundo mbinu ya uwezeshaji, mitaji, masoko na vipaumbele vya Serikali katika kukuza uchumi wa nchi. Programu nyingi zinazoanzishwa za uwezeshaji zinajikita mijini na chache sana ndizo

zinazotoa huduma mijini kama vile huduma za fedha na mafunzo. Pia Programu ziende kwa mujibu wa maeneo husika ya uwezeshaji. Ongezeko la Idadi ya Watu linaweza kutumika kama fursa ya kusimamia masoko kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa kupitia programu za uwezeshaji. Kwa mujibu wa takwimu za makadirio ya Idadi ya watu kwa mwaka 2021, Zanzibar ina jumla ya watu 1,717,608 (Wanaume 837,034 na Wanawake 880,574).

#### 2.9.7 Wazee

Wazee wa Zanzibar kwa takwimu za makisio mwaka 2021 (71,711) ambao ni sawa na asilimia 4.1% ya idadi ya watu. Kundi hili la Wazee lina mahitaji mengi ya kiuchumi na linakabiliwa na changamoto za kiafya. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi inatambua mchango mkubwa katika kuendeleza sekta hii pamoja na kushirikishwa katika programu za uwezeshaji kiuchumi.

## SURA YA TATU

## 3.0 DIRA, DHAMIRA NA KANUNI ELEKEZI ZA SERA

### 3.1 Dira

Kuwa na jamii iliyowezeshwa na kuimarika kiuchumi na kijamii kupitia fursa za uwezeshaji.

### 3.2 Dhamira

Kuimarisha uwezo wa Wazanzibari kutafuta, kuzitumia, kusimamia na kunufaika na fursa za kiuchumi kupitia uimarishaji wa utoaji wa huduma za uwezeshaji kwa kuweka mifumo na miundombinu wezeshi ya uwezeshaji, kuongeza uratibu wa upatikanaji wa mafunzo na masoko endelevu na ya uhakika, ushirikishwaji na upatikanaji wa mitaji pamoja na huduma za kifedha.

### 3.3 Lengo Kuu

Lengo kuu la Sera hii ni kuimarisha mazingira wezeshi ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuongeza tija, uzalishaji, ufanisi na masoko ya bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara nchini.

### 3.4 Malengo Mahususi

Sera itasimamia utekelezaji wa malengo mahsusi yafuatayo:-

1. Kuimarisha ushirikishwaji, upatikanaji wa mitaji na huduma stahiki na endelevu za kifedha;
2. Kuongeza na kuimarisha upatikanaji wa masoko na huduma zinazohusiana na masoko kwa bidhaa za Wajasiriamali;
3. Kuimarisha mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kuhamasisha utamaduni wa kijasiriamali, kuongeza ujuzi na kujenga uwezo wa Wadau na Wajasiriamali kuzalisha kwa ufanisi, ubora na tija;
5. Kuimarisha uratibu na muitikio wa sekta za uwezeshaji kiuchumi; na
6. Kuongeza upatikanaji wa miundo mbinu wezeshi, pamoja na huduma kwa Wajasiriamali wadogo na wakubwa.

### 3.5 Kanuni Elekezi za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

Misingi elekezi inawakilisha falsafa kuu ambayo inaelekeza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa Zanzibar kwa muda wote bila kujali mabadiliko ambayo yanaweza kutokea wakati wa utekelezaji wa malengo na mikakati yake katika ngazi zote za Serikali. Kanuni elekezi za Sera ni kwa ajili ya kuongeza fursa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi miongoni mwa watu wa Zanzibar~~.~~ zinazoongozwa na wajibu wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, Ibara ya 3 na Ibara ndogo ya 21 (3) inaeleza kuwa "Kila Raia wa Zanzibar anayo haki ya kufanya kazi", Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 imesisitiza juu ya "Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Raia wake". Dira ya Zanzibar 2050 na Mpango wake wa Utekelezaji mbali na mambo mengine inasisitiza kuimarisha upatikanaji wa fursa za Kiuchumi kwa jamii kupitia uwezeshaji wa jamii.

Nyaraka nyingine za kisheria za Kikanda na Kimataifa ni pamoja na Azimio la SADC la mwaka 1992, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2015 kwenye lengo la 1 na la 5 yanasisitiza suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi; Ajenda 2063 "Afrika Tuitakayo" eneo nambari moja linasisitiza Nchi W~~w~~anachama kuweka miundo mbinu na miongozo ya kusimamia uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Mkataba wa CEDAW wa mwaka 1979 Sura ya 3 Ibara ya 11 inaeleza kwamba "Nchi Wanachama watachukua hatua madhubuti kuhakikisha zinaondoa ubaguzi dhidi ya Wanawake katika nyanja za ajira ili kulinda usawa wa Wanawake na Wanaume, haki yenyewe inayostahiki hasa: haki ya kufanya kazi na Azimio la Beijing +10 la Wanawake la mwaka 2005 kipengele cha 2.2.1 kinasisitiza Uwezeshaji Kiuchumi na kuondoa Umasikini kwa Wanawake. Mbali ya kanuni zilizoainishwa hapo juu, Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utekelezaji wake utasimamiwa na misingi ifuatayo:-

**Kubadili fikra**: Kuna uhitaji wa haraka wa kuwawezesha Wanawake, Wanaume, Vijana, Wazee na Watu wenye Ulemavu wa Zanzibar kupitia mabadiliko thabiti ya kifikra ambayo yatalenga kuwezesha watu hawa ili waweze kufikiri kijasiriamali.

**Mtazamo chanya**: Mtazamo chanya unawasaidia Wazanzibari Wanawake, Wanaume, Vijana na Watu wenye Ulemavu kuona na kutambua fursa kwa Mzanzibar ambazo zitaweza kuwawezesha kiuchumi.

**Kujitolea**: Kuongeza Utayari na uchapakazi kwa kufanya vizuri ili kuwa na programu makini na yenye ufanisi ambayo itapelekea kuondoa umasikini.

**Kujikubalisha**: Inatarajiwa kwamba Wanawake, Wanaume, Vijana na Watu wenye Ulemavu kwa Zanzibar watakuwa imara, wenye maamuzi, malengo elekezi na kuwezeshwa.

**Uadilifu**: Ubora wa kuwa mkweli na kuwa na misingi imara ya maadili, ukweli, thamani na Unyoofu katika kutoa lengo linalotarajiwa.

**Uwazi:** Uzalendo na nia njema, ukweli na wenye kuaminika vya kutosha kubeba uchunguzi wa umma katika mambo yote ya uwezeshaji kiuchumi, programu na mikakati.

**Uratibu**: Muingiliano na Ushirikiano wa shughuli, majukumu, miundo ya uhamasishaji ~~kuchagiza~~ na kudhibiti, ili kuhakikisha kwamba rasilimali za Zanzibar zinatumika kwa ufanisi kulingana na malengo mahususi ya maendeleo.

**Ushirikiano**: Ni juhudi za kufanya kazi kwa pamoja, kwa lengo moja au kukamilisha kazi katika hali ya umakini na yenye ufanisi.

**Uwajibikaji:** Ni jukumu la mtu au Taasisi kukubali kuwajibika kwa niaba yao, na kubainisha/kufichua matokeo katika njia ya uwazi. Pia, inajumuisha kuwajibika katika majukumu ya kifedha au mali ulizoaminiwa.

**Weledi**: Mchanganyiko wa sifa zote ambazo zinaunganishwa na mafunzo, uzoefu, tabia na ujuzi wa mtu katika maeneo ya uwezeshaji kiuchumi.

**Ubunifu**: Kuanzishwa kwa wazo jipya/njia mpya yenye kulenga uundaji wa kufikiri ambayo itasababisha kuimarika kwa bidhaa/huduma au mazingira ya kazi kwa tija na ufanisi.

**Utawala Bora**: Programu za Uwezeshaji lazima inufaishe watu wote hususan wale wa ngazi za chini na wapatiwe haki na mwenendo wake uonekane.

## SURA YA NNE

## 4.0 HOJA, MATAMKO NA MIKAKATI YA SERA

### 4.1 Hoja ya Sera

***Kukosekana kwa Taasisi moja na sheria inayosimamia na kuratibu shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.***

#### 4.1.1 Tamko la Sera

Serikali itaundaa Taasisi maalum itakayosimamia uratibu na utekelezaji wa shughuli zote za uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

#### 4.1.2 Mikakati ya Sera

1. Kuanzisha Taasisi ya kitaifa itakayosimamia Uandaaji na Uratibu wa Shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Kuratibu uandaaji wa Mifumo ya Kisheria, Miongozo na Muundo wa kusimamia uendeshaji wa shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
3. Kuunda Bodi itakayosimamia uratibu na utekelezaji wa shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kusimamia upatikanaji wa rasilimali watu na rasilimali fedha kutekeleza shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
5. Kuanzisha na kuweka Mifumo ya Uratibu, Ripoti, Ufuatiliaji na Tathmini ya kusimamia utekelezaji wa Shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa ngazi zote;
6. Kuimarisha ufanyaji wa tafiti na upatikanaji wa takwimu sahihi kwa maendeleo ya sekta ya uwezeshaji nchini;
7. Kujenga Uwezo wa Taasisi na Wadau katika kusimamia shughuli na programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na
8. Kusimamia Uwezeshaji wa Wazawa katika miradi ya kimkakati na miradi ya uwekezaji nchini.

### 4.2 Hoja ya Sera

***Upatikanaji mdogo wa mitaji ya kuimarisha miradi na biashara za Wajasiriamali wadogo na wa kati.***

#### 4.2.1 Tamko la Sera

Serikali itaweka Mifumo na Miundo mbinu imara ya upatikanaji wa mitaji ya kutosha na mafunzo ya huduma za kifedha kwa Wajasiriamali wadogo na wa kati.

### 4.2.2 Mikakati ya Sera

1. Kuanzisha na Kuimarisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuweza kutoa mitaji na kusimamia upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo na wa kati;
2. Kuiunganisha Mifuko yote ya Uwezeshaji iliyopo nchini ili kuweza kutoa huduma kwa ufanisi;
3. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Huduma za Fedha kwa Wajasiriamali Wadogo na Kati ya mwaka 2019;
4. Kuimarisha utoaji wa mafunzo ya huduma za Kifedha na matumizi fanisi ya mitaji kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara ili wazalishe kwa faida;
5. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi za kifedha kutoa huduma za kifedha kwa wajasiriamali na wafanyabiashara;
6. Kuunganisha Wajasiriamali na Wafanyabiashara kwenye Benki za Kibiashara na Taasisi nyengine za Kifedha ili kupata mitaji ya kuendesha shughuli zao;
7. Kuziimarisha SACCOS kwa ajili ya kutoa huduma za kifedha endelevu kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara; na
8. Kuhamasisha Makampuni kusaidia Wajasiriamali wabunifu na wenye mawazo ya biashara kuendeleza biashara zao.

### 4.3 Hoja ya Sera

***Kutokuwepo kwa masoko ya uhakika kwa bidhaa za Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogowadogo, wadogo na wa kati ndani na nje ya nchi.***

### 4.3.1 Tamko la Sera

Serikali itasimamia upatikanaji wa masoko wa bidhaa za Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogowadogo, wadogo na wakati ndani na nje ya nchi;

### 4.3.2 Mikakati ya Sera

1. Kuanzisha Makongano na Mitandao ya Wajasiriamali kulingana na bidhaa wanazozalisha;
2. Kuimarisha Mnyororo wa thamani kwa bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia malighafi zinazo zalishwa na zisizozalishwa nchini;
3. Kuimarisha uwekezaji wa viwanda vidogo vidogo na vya kati vitakavyozalisha kwa kutumia rasilimali zinazozalishwa nchini;
4. Kuanzisha Kituo cha taarifa na tafiti za masoko na kuwaunganisha wajasiriamali na masoko ya ndani na nje ya nchi;
5. Kuimarisha Taasisi ya kusimamia na kuratibu masuala ya viwango na upatikanaji wa masoko yenye tija kwa bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara;

6. Kuandaa na kuimarisha ufanyaji wa Maonesho mbali mbali ya Biashara nchini na kuhamasisha Wajasiriamali kushiriki katika Maonesho nje ya Nchi;
7. Kuimarisha vyama vya ushirika nchini katika kuendeleza masoko ya bidhaa za wajasiriamali;
8. Kuweka Mikakati na kuhamasisha matumizi ya Bidhaa za ndani pamoja na kuihuisha 'Brand' ya bidhaa za Zanzibar (Made in Zanzibar);
9. Kuimarisha na kusimamia mifumo rafiki ya kisera na kisheria itakayowezesha kulinda soko la ndani la bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo, wadogo na wa kati;
10. Kuweka mazingira wezeshi kwa sheria za manunuzi kwa makusudi zinatoa fursa kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo, wadogo na wa kati ili waweze kuingia katika utoaji wa huduma;
11. Kuweka miundo mbinu imara ya masoko nchini; na
12. Kuimarisha utumiaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano katika kukuza soko la bidhaa za Wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo, wadogo na wa kati.

## 4.4 Hoja ya Sera

***Uhaba wa Elimu na Mafunzo ya Ujasiriamali, Biashara na Uwezeshaji yanayoendana na mahitaji ya soko la ajira na masoko ya bidhaa.***

### 4.4.1 Tamko la Sera

Serikali itahakikisha inasimamia upatikanaji wa Mafunzo Sahihi na yenye tija ya Ujasiriamali, Biashara na Uwezeshaji.

### 4.4.2 Mikakati ya Sera

1. Kuhamasisha uanzishwaji wa somo la ujasiriamali katika Mitaala ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika ngazi zote tokea Elimu ya Msingi;
2. Kuimarisha upatikanaji wa mafunzo sahihi ya ujasiriamali, mafunzo ya amali na mafunzo kazi kwa jamii hasa Vijana ya nadharia na vitendo yanayoendana na mahitaji ya bidhaa na soko la ajira;
3. Kujenga na kuhamasisha utamaduni wa kijasiriamali kwa jamii ikiwemo kubadilisha mawazo hasi juu ya upatikanaji wa ajira Serikalini;
4. Kuhamasisha uandaaji wa miongozo, mitaala na nyenzo maalum za kusimamia mafunzo ya ujasiriamali, biashara, masoko na ubunifu nchini;
5. Kuhamasisha, kuratibu na kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi endelevu na zenye tija kwa jamii;

6. Kuweka mikakati ya kuchangia gharama za mafunzo ya uwezeshaji, mafunzo kazi na ujasiriamali hasa kwa Vijana; na

7. Kuimarisha upatikanaji wa miundo mbinu sahihi na programu za kukuza vipaji na ubunifu nchini.

### 4.5 Hoja ya Sera

***Uhaba wa Miundombinu ya Mifumo ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.***

#### 4.5.1 Tamko la Sera

Serikali itaweka Miundombinu sahihi na ya kutosha ya kusimamia mafunzo, mitaji na masoko kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara ndogondogo na wa kati nchini.

#### 4.5.2 Mikakati ya Sera

1. Kuweka Miundombinu ya kutosha katika ngazi ya Taifa na Wilaya kusimamia masuala ya mafunzo ya Ujasiriamali na Biashara ikiwemo vituo vya kulea wajasiriamali, vyuo vya amali, EBDS na vyuo vya mafunzo kazi;
2. Kuanzisha, kuimarisha na kuhamasisha vituo vya ubunifu kwa jamii hasa Vijana ili kukuza ujasiriamali na uwezeshaji;
3. Kuanzisha vizimba vya biashara, masoko, sehemu za kuhifadhi bidhaa, viwanda na vituo vya maonesho kwa Mfumo wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kila Wilaya;
4. Kuimarisha Miundombinu ya Uwezeshaji itakayo zingatia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu na mahitaji maalum;
5. Kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme, mawasiliano na huduma za kifedha hasa vjijini ili kuvutia wawekezaji kuwekeza miundombinu ya uwezeshaji vijijini;
6. Kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vya vifungashio nchini kwa bidhaa mbali mbali za wajasiriamali; na
7. Kuhamasisha uzalishaji wa nishati mbadala hasa sehemu ambazo hazijafika Gridi ya Taifa ili kuimarisha uzalishaji na ujasiriamali.

### 4.6 Hoja ya Sera

***Uzingatiaji mdogo wa jinsia, Watu wenye Ulemavu, na mahitaji maalum katika kutoa fursa za Ujasiriamali, Uwezeshaji na Biashara.***

#### 4.6.1 Tamko la Sera

Serikali itahamasisha na kuhakikisha fursa za uwezeshaji wananchi kiuchumi zinazingatia jinsia, watu wenye mazingira na mahitaji maalum.

#### 4.6.2 Mikakati ya Sera

1. Kuhamasisha uanzishwaji wa Programu za Uwezeshaji zinazotoa fursa za ushiriki wa makundi yote wakiwemo Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu;

2. Kuhamasisha ushiriki wa Wanawake, Vijana na ujumuishwaji wa Watu Wenye Ulemavu katika Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi; na

3. Kuweka mazingira wezeshi kwa Programu za kuwawezesha Wananchi Kiuchumi ili ziweze kuzalisha fursa za ajira na kuondoa tatizo la ajira nchini hasa kwa Vijana, Wanawake na Watu wenye Ulemavu.

## SURA YA TANO

## 5.0 UTARATIBU WA KITAASISI KATIKA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ZANZIBAR

### 5.1 Mfumo wa Kitaasisi Katika Utekelezaji wa Sera

Wizara inayohusika na masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itaandaa na kutoa miongozo ya kisera na kisheria pamoja na kuweka viwango/vigezo vya kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mashirikiano ya karibu na Wahusika wengine muhimu wakiwemo Wizara za Serikali, Idara na Wakala wake; Sekta Binafsi; Vyombo vya Habari, Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo. Kwa kuimarisha utekelezaji mzuri wa Sera hii, Wizara yenye dhamana ya masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (kupitia Taasisi itakayoanzishwa) itakuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera na kusimamia uzingatiaji wa shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Sera, Programu, Mikakati na Bajeti mbali mbali za Kitaifa na Kisekta. Aidha, Taasisi hii ina jukumu la kutayarisha utaratibu wa Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kufuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa mikakati ya Sera. Sambamba na hilo, Mfumo wa kisheria wa kusimamia utekelezwaji wa Sera utawekwa.

### 5.2 Muundo wa Kitaasisi

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha Wizara maalum inayosimamia na kuratibu utekelezaji wa Shughuli na Program za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi nchini. Kwa Muktadha wa utekelezaji wa Sera hiiWizara pamoja na mambo mengine itaratibu uimarishwaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao utakuwa chini ya Wizara inayosimamia shughuli na Progrmu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Muundo wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utajumuisha uwepo wa Bodi ambayo ndio itakuwa msimamizi mkuu wa shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Taasisi hii itakuwa na Mkurugenzi Mtendaji ambaye atasimamia shughuli na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi chini ya maeneo makuu manne ambayo ni eneo la Mipango na Rasilimali Watu, Eneo la Programu na Mafunzo, Eneo la Huduma za Masoko na Eneo la Mitaji. Maeneo yote haya yatasimamiwa na Wakurugenzi wa ndani, Meneja na Watendaji wengine kwa mujibu wa mahitaji ya muundo. Eneo la Mipango na Rasilimali Watu litasimamia Mipango, Uendeshaji na Utumishi, Sera, Sheria, Bajeti, Utafiti, Ufuatiliaji, Tathmini, Teknohama, Takwimu na Uratibu; Eneo la Programu na Mafunzo kwa

Wajasiriamali litashughulikia Programu na Mafunzo yote ya Ujasiriamali nchini. Sehemu ya Masoko itakuwa na Kitengo cha Kusimamia Uzalishaji na Ubora wa Bidhaa, Kitengo cha Taarifa za Masoko na Kitengo cha Kukuza Biashara na Matangazo (Promotion and Advertisement). Sehemu ya Mitaji itakuwa na Kitengo cha Uratibu wa Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi na Huduma nyengine za Kifedha nchini; kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kitengo cha Uratibu wa Mabenki ya Kibiashara. Mbali ya mambo mengine, Wakala utafanya kazi kwa ukaribu na Idara/Taasisi za Umma na Binafsi zinazohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuhakikisha uwepo wa uratibu mzuri katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na shughuli ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 5.3 Mfumo wa Kisheria

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utekelezaji wake utakwenda sambamba na utungwaji wa Sheria ambayo mbali na mambo mengine itatoa Muongozo wa Kisheria katika uanzishwaji, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za Wakala wa Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

### 5.4 Mfumo wa Uratibu

Mafanikio ya utekelezaji wa Sera na Mipango mbali mbali kwenye Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika ngazi ya kitaifa na ngazi za chini yanahitaji kuwa na Mfumo makini wa uratibu unaoshirikisha Wadau wa sekta mbali mbali ikiwemo Wizara, Idara na Wakala kwa Sekta za Umma na Binafsi, Asasi za Kiraia na Washirika wa Maendeleo katika utekelezaji wa Sera hii.

Kutakuwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utakaokuwa chini ya Wizara inayosimamia Shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Wakala huo utakuwa ni sehemu ya uratibu na utendaji kwa Shughuli za Uwezeshaji Kiuchumi Zanzibar na ndio mratibu mkuu wa utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, program, mipango na mikakati yake katika ngazi zote. Vile vile, kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi wa Shughuli za Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambayo pamoja na mambo mengine itasimamia na kupitia taarifa za utekelezaji wa Sera, Shughuli na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kila robo mwaka kabla ya kuwasilishwa katika vyombo vya juu vya maamuzi.

Aidha, kutakuwa na Kamati ya Uongozi ambayo Mwenyekiti wake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Wajumbe ni Wakurugenzi wa Idara zote za Wakala. Kamati itakuwa na uwezo wa kumualika Mjumbe kutoka Sekta tofauti za Serikali na Binafsi ambayo itaratibu na itasimamia utekelezaji wa Sera na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kupitia Taasisi zao. Kamati hii itakutana kila baada ya mwezi.

Katika ngazi ya Wilaya, kutakuwa na Kamati za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambazo zitakuwa zinajumuisha wajumbe kutoka sekta mbalimbali zilizomo katika Wilaya hiyo. Wajumbe wa Kamati hizo ni wawakilishi wa sekta husika za kuwezesha wananchi kiuchumi katika ngazi za Wilaya ambapo kazi yao ni kuangalia utekelezwaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa Wilaya husika. Kamati hii itakutana kila mwezi na kuripoti kazi zake katika Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kila baada ya miezi mitatu kwa ngazi ya Wilaya husika. Katibu wa Kamati hii atakuwa ni Afisa kutoka kwenye dawati la masuala ya Uwezeshaji la kila Wilaya.

## 5.5 Majukumu ya Wadau katika Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar

Ili kutekeleza kikamilifu Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi mashirikiano baina ya Taasisi za Umma na za Binafsi, Asasi za Kiraia, Washirika wa Maendeleo na Jamii kwa ujumla yanahitajika. Wakala itawajibika na utayarishaji wa mifumo ya utekelezaji wa Sera ambayo itaelezea jukumu la kila Taasisi na Mdau katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar. Kila Taasisi itapewa kazi zake na majukumu yake katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Taasisi hizo ni kama zifuatazo:

### 5.5.1 Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

1. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kisera, kisheria na miundo sahihi ya kuratibu masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwemo Sera, Sheria na Miongozo;
2. Kutoa miongozo inayohusiana na masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
3. Kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kushajihisha upatikanaji wa rasilimali fedha za ndani na za nje ya nchi kwa ajili ya utekelezaji wa Programu za Uwezeshaji Kiuchumi;

5. Kuratibu mashirikiano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, katika kusimamia shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na
6. Kushajihisha wananchi kuzitumia fursa za uwekezaji zilizopo katika kuimarisha uwezeshaji wananchi kiuchumi.

### 5.5.2 Majukumu ya Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

1. Kutoa Ushauri kwa Serikali, Taasisi za Umma na Binafsi juu ya masuala yote yanayohusiana na kuimarisha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Kuratibu upatikanaji wa programu za mafunzo, programu za uwezeshaji, upatikanaji wa masoko, mitaji pamoja na kuwaunganisha wajasiriamali na wafanyabiashara na Taasisi za kifedha;
3. Kuimarisha uratibu na mashirikiano ya Wadau wa Kitaifa Kikanda na Kimataifa katika kutekeleza majukumu ya Wakala kwa ufanisi;
4. Kuimarisha masuala ya utafiti na ubunifu katika masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kukuza mahusiano na Taasisi za utafiti;
5. Kushirikiana na kuingia katika ubia na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa kwa ajili ya utekelezaji bora wa Mamlaka;
6. Kuanzisha na kuimarisha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za shughuli za uwezeshaji wananchi Kiuchumi za Kisekta pamoja na kusambaza taarifa kwa Wadau;
7. Kupendekeza njia na hatua za kuchukuliwa kuhakikisha kuwa huduma za kifedha kwa wajasiriamali zinapatikana;
8. Kupanga Mipango, Bajeti, kujenga uwezo wa Wakala na kusimamia upatikanaji wa rasilimali watu na fedha kwa uendeshaji waWakala;
9. Kumsajili au kumfuta Mjasiriamali au Mfanyabiashara;
10. Kushajiisha kuweka Akiba na Uwekezaji;
11. Kuchunguza na/au kukagua nyaraka zinazohusiana na mwenendo wa mjasiriamali au mfanyabiashara;
12. Kuandaa, kusimamia na kuratibu utekelezaji pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya program za uwezeshaji wananchi kiuchumi zilizopo; na
13. Kuimarisha na kuendesha Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 5.5.3 Bodi ya Wakurugenzi ya Wakala

1. Kuwa ni Msimamizi Mkuu wa shughuli za Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Kuratibu upangaji wa Mikakati, Mpango Kazi na Kusimamia utekelezaji wa shughuli

za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;

3. Kutafuta rasilimali fedha, vifaa na watu ili kuhakikisha shughuli za Wakala zinatekelezwa kwa ufanisi mkubwa;
4. Kusimamia na kupitisha ada zote zinazowekwa na Wakala kwa ajili ya huduma mbali mbali;
5. Kuzipitisha kwa ushauri wa Mheshimiwa Waziri Sera na Miongozo yote yanayohusiana na uendeshaji wa Wakala;
6. Kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
7. Kuzipitia taarifa zote za utekelezaji wa shughuli za Wakala kabla ya kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri; na
8. Kuishauri Serikali kupitia Wizara juu ya Maendeleo yaWakala.

#### 5.5.4 Wizara inayohusika na Fedha

1. Kutenga na kutoa rasilimali fedha na kufanya zipatikane kwa ajili ya utekelezaji wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Kuimarisha mahusiano imara na Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa matumizi stahiki ya rasilimali fedha; na
3. Kusimamia utekelezaji wa sheria na kanuni za fedha na manunuzi ili kusaidia wajasiriamali, wafanyabiashara na makampuni ya ndani yanayomilikiwa na wajasiriamali katika kutoa huduma mbalimbali na matumizi ya Serikali.

#### 5.5.5 Tume ya Mipango.

1. Kupitia na kuimarisha Mipango na Mikakati ya Maendeleo ya Taifa na Sera ya Serikali za Mitaa katika kukidhi mahitaji ya Wanawake, Wanaume, Wavulana, Wasichana na Makundi mengine yenye mahitaji maalum katika masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi;
2. Kuhakikisha masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi yanaingizwa katika mipango ya maendeleo ya Serikali za Mitaa, Wilaya, Sekta na Taifa;
3. Kuingiza masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika mfumo wa uchumi kwa kutumia moduli za uzingatiaji masuala ya kijinsia; na
4. Kukusanya taarifa za kitaifa juu ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

#### 5.5.6 Wizara inayohusika na Uchumi wa Buluu na Uvuvi

1. Kufanikisha uingizaji wa masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Sera ya Uchumi wa Buluu, Sera ya Uvuvi, Sera ya Mafuta na Gesi, Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Sekta hizo;
2. Kutengeneza mazingira wezeshi kwa wavuvi kupata teknolojia, mbinu na misaada ya uvuvi;
3. Kuimarisha mahusiano baina ya sekta binafsi na wavuvi, wakulima wa mwani na wakulima wadogo na wazalishaji wa mazao ya baharini katika masuala ya masoko;
4. Kutengeneza mazingira rafiki ya kuhamasisha Vijana kujiingiza katika sekta zilizo chini ya uchumi wa buluu, uzalishaji wa mwani, mafuta na gesi na kampuni za uvuvi;
5. Kuhamasisha biashara ya mazao ya uvuvi, mwani, ufugaji wa samaki, na programu za kuongeza thamani kwa bidhaa hizo;
6. Kuratibu mifumo ya kuhifadhi, kusarifu, kudhibiti ubora wa mazao ya uvuvi;
7. Kuanzisha viwanda vya kusarifu bidhaa na miundombinu ya kuhifadhi bidhaa za uvuvi, kilimo, ufugaji; Kuwahamasisha wajasiriamali wazichangamkie fursa zinazotokana na mafuta na gesi;
8. Kujenga uwezo kwa wavuvi wadogo wadogo kujihusisha na uvuvi wa bahari kuu;
9. Kufanikisha matumizi ya teknolojia ya juu iliyoboreshwa ili kupata rasilimali za baharini;
10. Kuhamasisha teknolojia ya usindikaji samaki miongoni mwa wavuvi wadogo wadogo; na
11. Kuandaa mazingira wezeshi kwa Vijana kujiajiri katika uvuvi, mafuta na gesi na mwani.

#### 5.5.7 Wizara inayohusika na Ufugaji na Kilimo

1. Kufanikisha uingizaji wa masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika Sera ya Kilimo, Sera ya Mifugo na Sera ya Misitu, Mipango na Miradi ya Maendeleo ya Sekta hizo;
2. Kutengeneza mazingira wezeshi kwa wavuvi na wakulima wadogo wadogo kupata teknolojia, mbinu na misaada ya uvuvi na kilimo;
3. Kuimarisha mahusiano baina ya sekta binafsi na wakulima wadogo na wazalishaji wa na wafugaji katika masuala ya masoko;

4. Kutengeneza mazingira rafiki ya kuhamasisha Vijana kujiingiza katika sekta kilimo na ufugaji;
5. Kuhamasisha biashara ya mazao ya kilimo na programu za kuongeza thamani kwa bidhaa hizo;
6. Kufanikisha uasili wa teknolojia ya kilimo na mifumo ya ubunifu ya kupunguza hasara baada ya mavuno;
7. Kuanzisha viwanda vya kusarifu bidhaa na miundombinu ya kuhifadhi bidhaa za kilimo na ufugaji; na
8. Kuwezesha wafugaji kuboresha uzalishaji na soko la bidhaa zao.

#### 5.5.8 Wizara inayohusika na Biashara na Viwanda

1. Kuratibu programu za maendeleo ya uanzishaji wa viwanda vidogo na vya kati kwa wajasiriamali na wafanyabiashara;
2. Kupanua nguvu ya mashirikiano na maafikiano/mapatano baina ya makampuni/wafanyabiashara wadogo wadogo;
3. Kusaidia kuimarisha viwango vya bidhaa za wafanyabiashara na wajasiriamali ili kuimarisha masoko ya bidhaa ndani na nje ya nchi;
4. Kusimamia upunguzaji wa gharama za viwango na ada za upatikanaji wa alama za ubora kwa bidhaa za wajasiriamali na wafanyabiashara; na
5. Kufanikisha urasimishaji wa biashara.

#### 5.5.9 Wizara inayohusika na Elimu

1. Kuimarisha ubora na kupanua upatikanaji wa mafunzo ya elimu na ufundi miongoni mwa Vijana wa Zanzibar;
2. Kuchochea fikra chanya juu ya ujasiriamali miongoni mwa wavulana na wasichana maskuli;
3. Kuhamasisha elimu ya kujitegemea kwa kuanzisha "Michepuo" katika maeneo ya kilimo, uvuvi, utalii na maeneo mengine;
4. Kupitia mtaala uliopo wa somo la maendeleo ya ujuzi wa kijasiriamali na kuufanya uwe wa lazima kwa Taasisi zote za elimu ya juu na zote zinazotoa elimu ya ufundi na ufundi stadi;
5. Kuimarisha elimu ya ufundi na vituo vya amali katika kukuza shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
6. Kukuza vipaji na ubunifu; na

7. Kushirikiana na Wakala kutoa ujuzi kwa mujibu wa mahitaji mbali mbali.

#### 5.5.10 Wizara inayohusika na Vijana na Wanawake

1. Kushawishi Wanawake na Vijana kujihusisha katika shughuli za kujiingizia kipato.
2. Kubadili mtazamo /fikra potofu za Vijana na Wanawake kuwa ujasiriamali ni moja kati ya kazi zisizokuwa za lazima;
3. Kuratibu na kufuatilia program na mifumo ya Uwezeshaji Kiuchumi kwa Vijana na Wanawake;
4. Kushawishi Vijana na Wanawake kujiunga katika Vyama vya Ushirika;

#### 5.5.11 Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ

1. Kutekeleza programu na shughuli nyengine zinazohusu Uwezeshaji Kiuchumi (ikiwemo kutenga fedha kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu);
2. Kuratibu na kufuatilia Programu za Uwezeshaji Kiuchumi kwa maeneo yao;
3. Kuzitambua na kuyaelewa maeneo muhimu yenye fursa za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuweza kuzitumia kwa maendeleo ya jamii;
4. Kusimamia uendeshaji wa miundombinu ya uwezeshaji wananchi kiuchumi itakayoanzishwa katika maeneo yao;
5. Kuanzisha Kamati za Uwezeshaji ambazo zitaongeza na kufanikisha maendeleo ya wajasiriamali/ujasiriamali;
6. Kusaidia uundwaji wa mitandao ya sekta maalumu ili kuongeza viunganishi vya biashara;
7. Kuweka mifumo ya ada zinazolipika kusaidia maendeleo ya wajasiriamali wa chini na wadogo; na
8. Kushawishi na kusaidia Vijana, Wanawake na makundi mengine yenye uhitaji kujishughulisha katika shughuli za kiuchumi.

#### 5.5.12 Wizara inayohusika na Utalii

1. Kuunganisha sekta ya utalii na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
2. Kutoa uelewa kwa jamii juu ya fursa zilizopo za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi katika sekta ya utalii;
3. Kusaidia uundwaji wa mtandao wa sekta mahsusi kuendeleza uhusiano kati ya wafanyabiashara, masoko na viwanda; na
4. Kujenga mazingira wezeshi kwa Vijana ili kuweza kuajiriwa na kujiajiri wenyewe katika sekta ya utalii.

### 5.5.13 Wizara inayosimamia Watu wenye Ulemavu.

1. Kuratibu upatikanaji wa mitaji, mikopo, mafunzo, programu na masoko kwa bidhaa za Wajasiriamali na kuwanyanyua kimaisha;
2. Kuhakikisha upatikanaji wa haki za ajira na kuweka miundo mbinu sahihi kwa Watu wenye Ulemavu kuzitumia fursa mbali mbali za uwezeshaji; na
3. Kuweka Programu za uwezeshaji kwa mujibu wa Watu wenye Ulemavu na makundi maalum.

### 5.5.14 Wizara inayohusika na Afya

1. Kusaidia SMEs hasa wanaojishughulisha na uuzaji wa vyakula kuzingatia masuala ya afya;
2. Kutoa ujuzi wa lishe na elimu ya afya kwa umma ili kuwa na taifa lenye afya;
3. Kuunganisha masuala ya afya na Programu za Uwezeshaji Kiuchumi;
4. Kuishawishi/kuhamasisha jamii kuwekeza kwenye Bima za Afya;
5. Kufanya uangalizi/ukaguzi/upimaji wa afya wa mara kwa mara kwa SMEs na sekta binafsi; na
6. Kuhamasisha wawekezaji kuwekeza kwenye huduma za afya kwenye shughuli zilizo mbali na mikondo ya pwani.

### 5.5.15 Sekta Binafsi

1. Kukusanya na kutoa taarifa za masoko na biashara kwa wafanyabiashara wadogo;
2. Kuanzisha na Kusimamia vituo vya BDS;
3. Kuingiza Program za Uwezeshaji Wananachi Kiuchumi na shughuli nyengine zinazohusiana nazo katika mipango yao;
4. Kushirikiana na Wadau wengine kutengeneza na kupanua fursa za kibiashara kwa makampuni ya ndani;
5. Kuhamasisha ubia na mfumo wake kwa kusaidia upatikanaji wa soko;
6. Kusaidia mazao mchanganyiko na kuongeza thamani ili kujenga soko jipya kwa makampuni ya ndani yanayomilikiwa na wajasiriamali;
7. Kushawishi na kuwezesha uundwaji wa biashara kupitia zile zilizoanzishwa na wawekezaji wakubwa wenye mitaji mikubwa; na
8. Kuunga mkono wale wote wanaoonesha mfano wa kuigwa katika sekta za biashara.

#### 5.5.16 Asasi za Kiraia

1. Kushirikiana na Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na sekta nyingine na wadau kuwezesha jamii kiuchumi;
2. Kushawishi na kuhakikisha kuwa masuala yote ya Uwezeshaji Kiuchumi yanaingizwa katika mipango, program na Sera za Taifa pamoja na ya kisekta. Kushiriki katika kufuatilia utekelezwaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Kiuchumi na mipango yake kupitia tathmini ya utoaji huduma shirikishi na ufuatiliaji wa rasilimali;
3. Kuimarisha mtandao miongoni mwa AZAKI katika kuhamasisha na kutekeleza Program za Uwezeshaji Kiuchumi na shughuli nyengine zinazohusiana nazo; na
4. Kutetea na kushawishi mabadiliko ya Sheria, mapitio ya Sera, na marekebisho ya mikataba ya kimataifa na makubaliano/utiaji saini katika kusaidia Uwezeshaji Kiuchumi kwa jamii.

#### 5.5.17 Vyombo vya Habari

1. Kushawishi uelewa wa jamii juu ya programu na shughuli nyengine zinazohusu Uwezeshaji Kiuchumi;
2. Kusimamia umuhimu ~~ya~~ wa Vyombo vya Habari katika kubadili fikra za Wananchi na kuelekea katika kujihusisha kwenye biashara kwa ajili ya kuondoa umasikini;
3. Kuonesha ushuhuda wa mafanikio kwa Programu za Uwezeshaji na makampuni yaliyopiga hatua kwenye hili; na
4. Kushawishi dhima kuu ya maendeleo ya ujasiriamali katika maendeleo ya taifa na kuondoa umasikini.

#### 5.5.18 Taasisi za Kifedha

1. Kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha kwa MSMEs;
2. Kuhamasisha utamaduni wa kujiwekea akiba miongoni mwa watu kama chanzo cha mtaji kwa ajili ya uwekezaji;
3. Kutoa fedha/mfumo wa dhamana kwa ajili ya shughuli mbali mbali zinayosaidia makampuni/biashara za ndani;
4. Kujiingiza/Kujihusisha kwenye elimu ya fedha na uingizwaji wake kwenye sehemu zote walipo raia;
5. Kurahisisha taratibu na masharti (mazingira rafiki) kwa ajili ya mikopo;
6. Kuweka dirisha maalum kwa makundi ya watu wenye mahitaji maalum ambayo yanataka kuanza kufanya biashara; na

7. Kushirikiana na Serikali kutoa mikopo na mitaji kwa wajasiriamali wakubwa.

#### 5.5.19 Washirika wa Maendeleo

Kushirikiana kusaidia juhudi za Serikali na Wadau wengine katika kuimarisha masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama ujenzi wa Vituo vya amali na Vituo vya Kule na Kukuza Wajasiriamali.

## SURA YA SITA

### 6.0 Ufuatiliaji na Tathmini

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itatayarishiwa Mpango wa Utekelezaji utakaobainisha Malengo, Mikakati na Shughuli zitakazotekelezwa kufikia lengo Kuu na Dira ya Sera. Ili kuweza kupima na kufahamu kwa kina utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utaandaliwa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao utakwenda sambamba na Mpango wa Utekelezaji wa Sera. Viashiria vya kupima utekelezaji wa mikakati ya Sera vitaandaliwa ambavyo vitakwenda sambamba na Viashiria vya Dira 2050, MKUZA na Viashiria vyengine vya Mikakati ya Kimataifa na Kikanda vinavyosimamia utekelezaji wa masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuhakiki utekelezaji wa Sera na kuona ya kwamba utekelezaji wa Sera una uwiano na Miongozo hiyo. Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini utaonesha Baseline na target kwa kila Kiashiria kitakachowekwa ili kuweza kujipima wakati wa kufanya tathmini. Masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera yatasimamiwa utekelezaji wake utafanywa na Idara ya Mipango na Utumishi ya Taasisi itakayoundwa kwa kushirikiana na Idara zitakazoratibu utekelezaji wa masuala ya mafunzo, mitaji na masoko kwa wajasiriamali.

### 6.1 Ufuatiliaji

Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itaweka bayana masuala ya Ufuatiliaji wa Shughuli zilizoainishwa katika Mpango wa Utekelezaji wa Sera. Mfumo wa Ufuatiliaji utabainishwa kwa kina katika Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini. Ufanisi wa utekelezaji wa Sera hii utakuwa unafuatiliwa kila Mwezi, miezi mitatu mitatu na kwa mwaka. Nyenzo za ufuatiliaji zitatayarishwa ili kurahisisha ufuatiliaji wake. Nyenzo za kukusanya Taarifa zitatayarishwa kutokana na viashiria vilivyopo katika Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Aidha, Ufuatiliaji utafanywa kwa mujibu wa Wadau Wakuu walioainishwa katika Sera ili kupima utekelezaji wa Majukumu yao yalioainishwa katika Sera. Pia, kutakuwa na Kamati za Uratibu zitakazokutana kwa mujibu wa muda uliopangwa zitatumika kama nyenzo ya kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera.Taarifa ya utekelezaji wa Sera itaandaliwa na kujadiliwa na Kamati za Uongozi ya Wizara na Kamati nyengine zilizoundwa kuratibu. Vile vile, Taarifa ya Utekelezaji wa Sera itawasilishwa kwa AMPR-SUB kwa hatua nyengine.

### 6.2 Tathmini

Ufanyaji kazi wa Sera hii utafanyiwa tathmini kila mwaka ili kuona kama imeleta matokeo yaliyotarajiwa kwa mujibu wa malengo na mikakati. Tathmini itafanyika kwa njia shirikishi na kuhusisha wadau wote muhimu. Pia, Tathmini nyengine itafanywa kila baada ya miaka mitatu ya utekelezaji wa Sera ili kuona kama ipo haja ya Sera kuendelea kufanyakazi au inahitaji kufanyiwa mapitio.

Mapitio ya Sera yatafanyika baada ya miaka mitano ili kuona kama Sera imefikia malengo na Dira yake na kama bado nini kifanyike. Ukomo wa utekelezaji wa Sera hii utakuwa ni kwa Miaka kumi tokea kuanza utekelezaji wake. Nyenzo za kufanya tathmini na mapitio zitatayarishwa.

### 6.3 Utaratibu wa Kuripoti

Kuripoti utekelezaji wa sera hii kunatazamiwa kuwa kipengele muhimu kwa mafanikio ya Uwezeshaji wa Kiuchumi kwa Wananchi.Wizara inayohusika katika kuratibu uwezeshaji kiuchumi itakuwa na jukumu kubwa la Kuripoti maendeleo ya utekelezaji wa Sera kwa AMPR-SUB na AMPR-SUB itawasilisha utekelezaji wa Sera katika Kikao cha Makatibu Wakuu na hatimae Baraza la Mapinduzi.

Wizara Inayohusika na Uwezeshaji wa Kiuchumi itaimarisha ripoti za mwezi na robo mwaka kutoka sekta mbali mbali kupitia Kamati za Kusimamia uratibu wa utekelezaji wa Sera zitakazoundwa. Ripoti itawasilishwa kwenye Kamati ya Uongozi ya Wizara inayohusika na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na hatimae kupelekwa kwenye ngazi nyengine za Maamuzi.

Kamati za Wilaya za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Kamati za Kutengeneza Ajira za Wilaya zitaripoti maendeleo yanayofanywa katika kutekeleza Sera hii kwa ngazi ya Wilaya na kwenyeTaasisi inayohusika na Kuratibu masuala ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

### 6.4 Mkakati wa Mawasiliano

Mkakati wa Mawasiliano wa Sera yaTaifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi utaandaliwa sambamba na utekelezaji wa Sera ambao utahusisha kusambaza maudhui ya Sera na taarifa za Utekelezaji wa Sera. Pia, utabainisha namna Wadau Wakuu wa utekelezaji wa Sera watakavyopata taarifa na nakala za Sera zitakavyosambazwa kwa Wadau ambapo baada ya Sera kupitishwa tu, Taasisi ya uratibu wa utekelezaji wa Sera itafanya mafunzo maalum na kuwaelewesha Wadau juu ya utekelezaji wa majukumu yao na kuwapitisha katika Sera kipengele kwa kipengele. Taarifa za utekelezaji wa sera zitasambazwa kwa jamii kupitia vyombo vya habari, mikutano na vijumbe maalum vitakavyoandaliwa. Kwa kuwa baadhi ya Wadau na wanufaika wa masuala ya Uwezeshaji ni pamoja na Watu wenye Ulemavu; Mkalimani wa lugha za Alama atatafutwa ili awepo katika mafunzo na huduma mbali mbali zitakazotolewa.

### 6.5 Mpango wa Rasilimali wa Sera

Mpango wa Rasilimali utakwenda sambamba na Mpango wa Utekelezaji wa Sera na Mpango wa Ufuatiliaji naTathmini. Utabainisha Rasilimali zinazohitajika katika kutekeleza kila Mkakati ulioainishwa katika Sera ili kuweza kusimamia masuala muhimu ya Uwezeshaji ikiwemo mikopo, mafunzo, ujasiriamali na upatikanaji wa mitaji. Mpango wa Rasilimali utaainisha gharama ikiwemo fedha, rasilimaliwatu, vifaa, teknolojia, ardhi, miundombinu na hata fidia inayohitajika. Mpango huu utaweka wazi gharama zote zinazohitajika katika utekelezajiwa Sera kipengele kwa kipengele.